

# Mwongozo Wa Mwalimu


6

## Kukua Kupitia Kufeli

Msamaha, urejesho na kupona kutokana na kufeli








# **Kukua Kupitia Kufeli**

**Msamaha, urejesho na kupona kutokana na kufeli**

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwalimu

Toleo la Tano



# **Kukua Kupitia Kufeli**

## **Msamaha, urejesho na kupona kutokana na kufeli**

Kimeandikwa Na David Batty  
Mwongozo Wa Mwalimu  
Toleo la tano

Maandiko Yanayotumiwa Katika Kitabu Hiki Yametoka Kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwa mtandao kwenye tovuti hii: [www.iTeenChallenge.org](http://www.iTeenChallenge.org) Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo:  
*Growing Through Failure, 5th edition*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* yanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, shuleni, katika huduma za gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vilevile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, cha Mwongozo Wa Somo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge  
PO Box 511  
Columbus, GA, 31902 USA  
Barua Pepe: [gtc@globaltc.org](mailto:gtc@globaltc.org)  
Tovuti: [www.globaltc.org](http://www.globaltc.org)  
[www.iTeenChallenge.org](http://www.iTeenChallenge.org)



Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 09-2023

# Kukua Kupitia Kufeli

Jambo moja la kawaida katika maisha ya Wakristo wapya ni kufeli. Wakristo wapya mara nyingi hujifunza kwamba “Wakristo hawapaswi kufeli,” hasa ikiwa wamejitolea kikamilifu kwa Kristo. Tutaangalia kufeli kwa makini katika kozi hii. Ni sehemu ya kawaida ya maisha ya kila mtu na Mungu ana la kusema kuhusu jinsi ya kukabiliana na kufeli na jinsi ya kuzuia kufeli.

## 1

### Sura ya 1. Sababu za kufeli kwangu

Somo hili linajumuisha kujifunza aina tofauti za kufeli na kile ambacho Mungu anafanya tunapofeli. Tunaangalia kwa karibu baadhi ya matatizo yanayosababisha kufeli.

## 2

### Sura ya 2. Hatua za kwanza za kupona kutoka kwa kufeli

Sura hii inalenga kile tunachopaswa kufanya tunapofeli. Pia, tunajadili miongozo ya kibiblia juu ya msamaha na urejesho kutoka kwa kufeli kwetu kwa zamani.

## 3

### Sura ya 3. Jinsi ya kukua kupitia kufeli kwangu

Sura hii inaangazia hatua tatu kuu za ukuaji zinazohusiana na kufeli kwetu. Kwanza, ukuaji wetu unapaswa kulenga kushinda matatizo yaliyosababisha kufeli kwetu. Pili, tunapaswa kujifunza jinsi ya kuishi maisha yenye afya. Tatu, tunapaswa kuchukua hatua za kuzuia kufeli tena.

## 4

### Sura ya 4. Kurudia tena uraibu

Je, kurudia ni nini? Ni nini kinachosababisha kurudia? Unawezaje kuzuia kurudia? Ishara za mapema za kurudia ni zipi? Unapaswa kufanya nini unaporudia? Tunaangazia masuala haya ili kujifunza kuepuka kufeli katika sehemu kubwa ya maisha yetu.

## Yaliyomo Katika Mwongozo Huu Wa Mwalimu

Kitabu hiki kina sehemu nne. Kila sehemu imeanza kwa ukurasa wenye rangi ya njano, ambao ni ukurasa ulio na jina la mada.

1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo
2. Mwongozo wa Mwanafunzi
3. Mwongozo Wa Somo
4. Mtihani Wa Mwanafunzi Na Cheti Cha Somo

Maelezo ya jinsi ya kutumia kila sehemu yanapatikana mara tu baada ya utangulizi wa ukurasa unaofuata.

# Utangulizi

Hili ni somo moja katika mfululizo wa masomo ulioandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha Wakristo wapya. Tunaamini kwamba lipo hitaji kubwa sana siku hizi la kuwasaidia Wakristo wapya ili wahusishe mafundisho ya Kristo na maisha yao ya kila siku kwa vitendo. Mafundisho haya pia yanaweza kutumiwa vizuri sana kwa ajili ya huduma kwa vijana kanisani na watu wazima wanaotamani kufanya Ukristo kuwa sehemu ya maisha yao kila siku.

Kusudi kubwa la somo hili na mfululizo mzima wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* ni kuwatambulisha Wakristo wapya kwa maswali muhimu yanayohusu maisha. Hatujaribu kuwapa mafundisho yatakayokuwa ndiyo mwisho kuhusu mada husika.

Kamati ya Mtaala ya Huduma ya Teen Challenge Marekani, ina mpango wa kuendelea kupitia upya na kufanya marekebisho kwa masomo haya. Tunakaribisha mawazo yoyote au hoja za kutusaidia kuyaboresha.

## Jinsi ya kutumia Mwongozo huu Wa Mwalimu

### 1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo

Kurasa za kwanza katika sehemu hii zinatoa mtazamo wa somo zima kwa ufupi.

Ukurasa unaofuata utakuwa ni nakala ya *Orodha Ya Kazi Za Darasani*. Hii orodha inaonyesha wakati ambapo kila zoezi katika Mwongozo wa Somo linatakiwa kukamilishwa, na wakati kila chemsha bongo na mtihamu zitatolewa. Kila mwanafunzi anapaswa kupewa habari stahiki kwa ajili ya ukurasa huo mwanzoni mwa kila somo. Kitabu hiki cha Mwongozo wa Somo tayari kina nakala isiyoandikwa chochote ya fomu hiyo, kwenye jalada la nyuma upande wa ndani.

Kitakachofuata ni mipango kwa ajili ya kufundishia kila somo. Hiyo yote ina kitu kinachoitwa Kweli Kuu ya Kibiblia pamoja na Mstari Mkuu. Hivyo vitu viwili vinaweza kutolewa mwanzoni mwa kipindi cha darasa. Pia vinasaidia kufanya mjadala ulenge yanayotakiwa kwa wakati wote.

Chini ya Kweli Kuu ya Kibiblia na Mstari Mkuu, kuna maelezo machache jinsi ya kufundisha somo lenyewe. Mara nyingi, marejeo yanaelekezwa kwa Mwongozo wa Mwanafunzi au kwa Zoezi linalopatikana katika Mwongozo wa Somo.

Kila somo humalizika kwa shughuli ya kufanya katika “Kufanyia Kazi Somo Maishani.” Umuhimu wa kipengele hiki hauelezeki. Wakristo wapya wanahitaji mwongozo ulio wazi kuhusu jinsi ya kuanza kufanyia kazi mafundisho haya katika maisha yao ya kila siku. Hakikisha kwamba una toa nafasi ya kutosha ili kuwasaidia wanafunzi wako kuanzisha shughuli hii.

Mwisho wa kila mpango wa kufundishia somo kuna orodha ya kazi za wanafunzi kufanya.

Mengi katika masomo haya yalikusudiwa kuwa na vipindi vitano vya darasa, kila kimoja kikitumia kwa saa moja. Kipindi cha mwisho darasani ni kwa ajili ya mtihamu. Masomo yote 14 katika mfululizo huu yanaweza kukamilishwa katika kipindi cha miezi kati ya mitatu hadi



minne, kama darasa litakutana kwa siku tano katika wiki. Ikiwa unafanya darasa kwa saa moja tu kwa juma, unaweza kukamilisha somo moja kwa mwezi – na mfululizo wote kwa kama mwaka mmoja. Mengi katika haya masomo yanaweza kupanuliwa na kufundishwa kwa muda mrefu, au kwa madarasa zaidi.

## 2. Mwongozo wa Mwanafunzi

Kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwanafunzi chaweza kutimiza makusudi mawili. Unaweza kutaka wanafunzi wasome kurasa husika katika kujiandaa kwa ajili ya somo linalofuata. Au, unaweza kuwataka wakisome baada ya wewe kufundisha somo, ili kufanya kama marudio na kuwa kama njia ya kuisitiza na kukazia kilichofundishwa darasani.

Tunakutia moyo uwaambie wanafunzi wajiandikie notsi darasani, hata ingawa utawapa Mwongozo wa Mwanafunzi. Wanayojiandikia wenyewe pamoja na mazungumzo na mijadala darasani vitawasaidia sana kuelewa vizuri baadhi ya mada zinazoshughulikiwa katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

## 3. Mwongozo Wa Somo

Mazoezi yaliyo katika Mwongozo wa Somo yameandaliwa ili kumpa mwanafunzi kazi ya kufanya nje ya darasa. Baadhi ya kazi-mradi hizo zinasaidia kumwandaa mwanafunzi kwa ajili ya somo la darasa linalofuata.

Mengi ya mazoezi haya yamekusudiwa kuwasaidia wanafunzi wajikite ndani zaidi na kutazama baadhi ya maswala yanayojadiliwa darasani kwa kina. Lengo kuu la kazi hizo nyingi ni kuwasaidia wanafunzi wagundue njia za kufanyia kazi hizo za kweli za Biblia katika maisha yao ya kila siku.

## 4. Mtihani Wa Mwanafunzi na Funguo la Majibu ya Mtihani

Mitihani hii imeandaliwa ili kutoa kipimo rahisi tu cha maendeleo ambayo kila mwanafunzi alipata katika uelewa wa kweli za Biblia zinazoshughulikiwa katika somo hili. Karatasi ya Majibu kwa ajili ya mtihani husika iko mara tu baada ya ukurasa wa mwisho wa ile nakala mfano ya mtihani wa mwanafunzi, katika Mwongozo huu wa Mwalimu.

## 5. Cheti Cha Somo

Cheti cha somo ni kwa ajili ya kuwatambua wale wanaomaliza kazi yote inayotakiwa kwa ajili ya somo hili na kufaulu mtihani. Mfano wa cheti hicho cha somo upo katika ukurasa wa mwisho wa kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwalimu. Cheti cha Kufuzu pia kinapatikana kwa wale wanafunzi wanaomaliza masomo yote 14 katika mfululizo huu wa *Mafunzo ya Vikundi Ya Maisha Mapya*. Pia, mfano upo katika kile kitabu kinachoitwa *Kuwatambulisha waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*.

## Jinsi Masomo Haya Yalivyotokea

Sulemani alisema, hakuna kitu kipya chini ya jua. Maneno hayo yanaweza kufaa hata kuhusu masomo haya. Mawazo yake mengi si mapya. Tunataka kutoa shukrani zetu maalum kwa Institute in Life Principles (Taasisi Ya Kanuni Za Maisha) kwa ushawishi mkubwa katika maisha ya watu waliotayarisha masomo haya. Masomo mengi yana alama za huduma hiyo ya Institute in Life Principles.

Nataka pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengi sana na maelfu ya Wakristo wanya ambao wametumia masomo haya katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita. Mawazo yao yamekuwa na mchango mkubwa sana katika maandalizi ya masomo haya. Pia ninamshukuru sana Ndugu Don Wilkerson kwa kunipa nafasi ya kufanya kazi katika kituo cha huduma ya Teen Challenge pale Brooklyn, New York, tokea mwaka wa 1971 hadi 1975. Katika miaka hiyo ndipo matayarisho yalipoanza ya masomo haya yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*.

Toleo la tano la *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* lilitayarishwa kwa msaada wa kamati ya Mitaala ya huduma ya Teen Challenge Marekani. Natoa shukrani maalum kwa wote waliosaidia katika mapitio na marekebisho hayo.

## Sera Kuhusu Kunakili Machapisho Haya

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi kinachohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* kinalindwa na Sheria za Haki Miliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali fulani, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kwenye mtandao kwa tovuti hii: [www.iTeenChallenge.org](http://www.iTeenChallenge.org) Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Dave Batty



## Pendekezo Kuhusu Mpangilio Wa Kufundisha

Somo hili ni moja kati ya 14 katika mfululizo wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*. Masomo yote 14 yameorodheshwa hapa kama pendekezo la jinsi ya kuyafundisha. Mfuatano huu ulitayarishwa kwa ajili ya ufundishaji endelevu wa masomo haya. Tunaweza kuutazama kama picha ya gudurumu lenye vyuma kumi na vinne. Masomo haya hayategemei linalotangulia. Kila somo linasimama lenyewe. Basi, mwanafunzi anaweza kujiunga na madarasa wakati wowote na akaingia tu vizuri kwenye mfumo.

1. Naweza je Kujua Mimi Ni Mkristo?
2. Kuitazama Biblia Kwa Haraka
3. Mitazamo
4. Majaribu
5. Maisha Ya Kikristo Yenye Mafanikio (ni pamoja na mafunzo juu ya huduma ya Roho Mtakatifu.)
6. Kukua kupitia kufeli
7. Matendo Ya Kikristo (Mahusiano Katika Kanisa La Mahali)
8. Utiifu kwa Mungu
9. Utiifu kwa Mwanadamu
10. Hasira na Haki za Kibinafsi
11. Jinsi Ya Kujifunza Biblia
12. Kujipenda na Kujikubali Mwenyewe
13. Mahusiano yako wewe Binafsi na Wengine
14. Nguvu Ya Kiroho na Mambo Yasio Ya Kawaida

Tazama kitabu kiitwacho, *Kuwatanguliza waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*, ili kupata maelezo zaidi juu ya kufundisha masomo hayo.



# Mipangilio ya Masomo Kwa Mwalimu

Angalia ukurasa wa 4 wa Mwongozo wa Mwalimu kwa habari zaidi  
kuhusu matumizi ya mipangilio hii ya masomo

## Muhtasari wa kozi hii

1. Unaweza kutanguliza kozi hii kwa wanafunzi siku moja au mbili kabla ya kipindi cha kwanza darasani na kuwapa kazi zao za kwanza. Zoezi la kwanza katika Mwongozo wa somo linapaswa kukamilika kabla ya kipindi cha kwanza cha darasa. Wape wanafunzi Mwongozo wao na uwaambie wasome Sura ya Kwanza, ambayo itajadiliwa katika kipindi cha kwanza darasani.
2. Kwenye ukurasa unaofuata katika mwongozo huu wa mwalimu kuna nakala ya ***Orodha ya kazi Darasani*** inayotoa tarehe ambayo kila kazi inapaswa kukamilishwa. Waagize kujaza tarehe zinazofaa kwenye nakala tupu katika ***Orodha ya kazi Darasani*** nyuma ya Mwongozo wao wa somo.
3. Kila mpangilio wa somo una “Zoezi la utangulizi wa somo” zaidi ya moja vitakavyotumika mwanzoni mwa somo hilo. Kusudi kuu la kufanya haya ni kuwasaidia wanafunzi kuwa makini katika mada kuu ya somo hilo. Tunataka kuunda mazingira mazuri na yenye uwazi yatakayowafanya wanafunzi wote kuhisi huru kushiriki katika majadiliano darasani.
4. Unapaswa kuamua ni vipindi vingapi vya darasa utakavyotumia kufundisha kozi hii. Kuna mipangilio ya masomo kwa vipindi 5 vya darasa (Cha 5 ni cha mtihani). Hata hivyo, ikiwa una muda wa kutosha unaweza kupanua kozi hii na kuwa vipindi zaidi. Somo la pili linahusiana na msamaha na urejesho. Unaweza kutumia kipindi tofauti cha darasa kwa kila moja ya mada hizi.
5. Katika kozi hii, kuna uwezekano wa wanafunzi kukata tamaa na kupata msongo wa mawazo wanapotafakari juu ya kufeli kwao zamani. Lengo kuu la kozi hii ni kuonyesha kuwa Mungu anaweza kuleta tumaini katika maisha yao licha ya kushindwa kwao kwa zamani. Tunataka wajue jinsi Mungu anaweza kuwaponya kutoka kwa kufeli kwao kwa zamani. Pia, tunataka kuwafundisha njia za kukabiliana na matatizo yanayoweza kutokea ili wasiendelee kufeli, hasa pale ambapo kufeli kunasababisha dhambi.
6. Kozi hii inayohusu kufeli inaweza kuelekezwa kwa urahisi kwa mahitaji ya msingi ya wanafunzi wako. Katika kozi hii, mifano mingi na mafundisho katika Mwongozo wa Mwanafunzi inahusiana na kufeli kwa wale wanaokabiliana na dawa za kulevya. Hata hivyo, kozi hii inatoa mafundisho kwa mtu yeyote ambaye amewahi au hajawahi kutumia dawa za kulevya. Kanuni hizi zinatumiwa kwa tatizo lolote linaloweza kudhibiti maisha pamoja na masuala ambayo watu wengine wanaweza kuona kama sio tatizo.
7. Suala lingine litakaloibuka kwa baadhi ya wale wanaofundisha kozi hii ni matumizi yetu ya maneno “kupona” na “kurudia.” Maneno haya yanaweza kuwa na maana iliyofungamana na mazoea fulani kwenye matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya kulingana na ujuzi wako. Elewa kwamba tumekuwa makini kufafanua jinsi tunavyotumia maneno haya. Tunapozungumzia kupona, hatuzungumzii tu hatua za kujisaidia kukabiliana na kufeli kwa zamani. Tunatambua haja ya uwezo wa Mungu wa kubadilisha ili kuleta mabadiliko makubwa katika maisha yetu.

Kuhusu “kurudia,” tumechagua kutumia neno hili badala ya “kurudi nyuma” kwa sababu wengi wa wanafunzi wa kawaida ambao watachukua darasa hili hawana asili ya ndani ya kidini. Tumejaribu kutumia lugha ambayo mtu wa kawaida ambaye sio Mkristo na pia Mkristo mpya wanaweza kuelewa. Hatujaribu kupuuza uharibifu wa kiroho unaotokea wakati mtu anarudia—ambao unaweza kujumuisha kuvunja mojawapo ya sheria za Mungu.

## Orodha ya kazi za Darasani

Mada ya Somo: Kukua Kupitia Kufeli

**Chemsha Bongo** Mstari wa kumbukumbu

Tarehe

1. Mathayo 6:14-15

Siku ya 2

2. Zaburi 32:8-9

Siku ya 3

3. \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

**Zoezi** Tarehe ya Kuwasilisha

1. Siku 1

2. Siku 2

3. Siku 3

4. Siku 4

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

**Mtihani** Tarehe Siku 5

## 1

## Somo 1 Sababu za Kufeli Kwangu

### 1. Kweli kuu ya Kibiblia

Ninapaswa kufahamu tatizo kuu maishani mwangu linalosababisha kufeli.

### 2. Mstari mkuu: Waebrania 4:16 Bibilia Takatifu (SUV)

Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

### 3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili

Sura ya kwanza katika Mwongozo wa Mwanafunzi inaenda pamoja na somo hili. Zoezi la 1 kwenye Mwongozo wa Somo, *Kuangalia Kufeli Mara ya Kwanza*, litatumika katika somo hili.

### 4. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5-10)

Waagize wanafunzi wajibu maswali 1-6 kutoka kwenye Mwongozo wa Somo, Zoezi 1, *Kuangalia Kufeli Mara ya Kwanza*. Tumia hiki kama chombo cha kuwafanya wawe makini kwa somo letu la leo-kufeli.

1. Je, Wakristo waliofaulu huwa wanafeli?
2. Je, kufeli kila mara huwa ni dhambi?
3. Toa mfano wa kufeli kukubwa kwa mtu fulani. (Inaweza kuwa ni kufeli kwako binafsi, au kwa mtu mwingine, kwa mfano, mwanasiasa.)
4. Je, Mungu hukasirika kila mara Mkristo anapofeli?
5. Je, umeshawahi kurejelea dhambi maishani mwako? (Kurejelea dhambi ina maana kuwa, baada ya kushinda tatizo au dhambi, unatumbukia kulitenda tena.)
6. Je, unajipima vipi kuhusu kuwa mshindi au mwenye kufeli?  
Alama zangu \_\_\_\_\_  
Jiwekee nambari kati ya 1 na 10. “Moja” inamaanisha kuwa unajichukulia kuwa umefeli kabisa. “Kumi” inamaanisha maisha yako daima yamejawa na ushindi pasipo na kufeli.

Kutoka Kukua Kupitia Kufeli Mwongozo wa Somo Zoezi 1, kuangalia kufeli kwa mara ya Kwanza

Chukua dakika 4-5 kujadili majibu yao kwa maswali haya. Kwa maswali 1, 2, 4 na 5, unaweza kuwauliza ni wangapi wamejibu “ndio” na ni wangapi walichagua “hapana.” Katika hatua hii, usijaribu kuzua mjadala wowote wa ni lipi lililo sahihi au lisilo sahihi. Eleza kwamba tutazungumzia maswala haya yote kwa undani zaidi katika kozi hii.

Swali la 3 limebuniwa ili kujifurahisha na kukupa mifano ya kutumia katika somo lote la leo.

Kwa kuwa swali la 5 na 6 kwenye Mwongozo wa Somo zoezi la 1 si ya kibinafsi kama mengine, unaweza kuwaomba wajitolee kutoa majibu yao kwa maswali haya. Unaweza kuwaambia waeleze kwa kifupi ni kwa nini walichagua jibu hilo –hata hivyo usiwaache kuibadili kuwa tawasifu ndefu ya maisha yao.

## 5. Lengo la leo—Sababu za kufeli

Eleza kuwa leo tutazungumzia sababu za kufeli kwako. Tunaweza kuzungumzia kwa kifupi jinsi ya kutatua baadhi ya matatizo, lakini sehemu hiyo ya kufeli itazunguziwa kwa undani zaidi katika masomo 2 na 3.

## 6. Jadili Hoja A. Aina tofauti za kufeli (dakika 5-10) . . . . . ukurasa wa 4-7, Mwongozo wa Mwanafunzi

Jadili aina tofauti za kufeli. Tumia muundo ulio kwenye ukurasa wa 4-7 wa Mwongozo wa Mwanafunzi kama mwongozo. Eleza kwa haraka kuwa kufeli kwingine ni dhambi na kwingine sio dhambi. Kisha waambie waorodheshe aina tofauti za kufeli ambazo zinafaa kuwa chini ya vichwa hivi vitatu vya jumla. Unaweza kutumia mifano waliyotoa kwa swali la 3 la Zoezi 1 kwenye Mwongozo wa Somo, kuelezea baadhi ya kufeli huku.

### Aina tatu za kufeli

1. Kufeli ambako sio dhambi
2. Kufeli ambako ni dhambi
3. Kufeli ambako husababisha dhambi

*Kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 4-7*

## 7. Kufeli ambako ni dhambi

Katika kujadili kufeli ambako ni dhambi, hakikisha wameelewa kwamba kulingana na mtazamo wa Mungu kila dhambi ni kufeli. Katika kozi hii juu ya kufeli, tutajadili kufeli ambako kuna faa kuwekwa katika kitengo hiki-Dhambi.

## 8. Jadili Hoja B. Mungu hufanya nini wakati kufeli kwangu ni dhambi? (dakika 5-10) . . . . . kurasa 7-8, Mwongozo wa Mwanafunzi

Jadili kile Mungu hufanya wakati unapofeli. Tazama ukurasa wa 7-8 za Mwongozo wa Mwanafunzi kwa maoni zaidi juu ya jambo hili. Pia, rejelea swali la 4 kwenye zoezi la 1 katika Mwongozo wa Somo ambalo tulijadili mwanzoni mwa kipindi cha darasa.

Hakikisha mwanzoni mwa sehemu hii unasisitiza kwamba Mungu anataka kutumia kushindwa maishani mwako kama fursa ya ukuaji.



## 1

Pia, unganisha majadiliano haya na sehemu iliyotangulia katika kufafanua vikundi 3 vya kufeli — kufeli ambako sio dhambi, kufeli ambako ni dhambi, na kufeli kunakosababisha dhambi. Onyesha kuwa majibu ya Mungu yatakuwa tofauti sana kulingana na kufeli.

Katika sehemu hii ya somo, tunataka kuangazia haswa jibu la Mungu wakati kufeli kwetu ni dhambi. Onyesha kwamba Mungu huhuzunika kila wakati mtu anapotenda dhambi — wakati mtu anashindwa kufuata sheria ambazo Mungu ametoa.

Onyesha kwamba wakati mwingine Mungu hukasirika na watu wanapotenda dhambi. Unaweza kutoa mfano mmoja au miwili kutoka kwa Biblia ili kuonyesha haya. Wakati mwingi, Yesu alipokasirishwa na watu ambao walikuwa wakifanya dhambi, hasira Yake ilielekezwa kwa wale waliosema kuwa ni wafuasi wa Mungu, lakini walikuwa wakipuuza sheria za Mungu wakijua. Dhambi hii ya kukusudia humkasirisha Mungu — kwa sababu mtu huyo anajua kilicho sawa, lakini anachagua kutokifanya.

Hakikisha unasisitiza maswala yaliyoibuliwa katika hoja ya 5 na 6 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi katika ukurasa wa 8 — kwamba Mungu ametupa sababu ya kuwa na matumaini katika siku zijazo, na Yeye yuko tayari kila wakati kukusaidia kukua unaposhindwa.

## 9. Je! Umeshindwa kabisa? (Dakika 2- 5)

Onyesha katika sehemu hii kuwa kuna tofauti kati ya kufeli na kujiona umeshindwa kabisa. Mungu huona kufeli kwako, lakini hakuoni kama uliyeshindwa kabisa. Wala, hupaswi kujiita aliyeshindwa kabisa.

Eleza kwamba Mungu huona uwezo wa kila mtu. Waefeso 2:10 inasema kwamba Mungu amemuumba kila mmoja wetu kufanya matendo mema. Yesu alipomwona mtu aliyepagawa na pepo huko Gadara, Aliona uwezekano wa mtu huyo kuwa mwinjilisti. Watu wengine waliona mwendawazimu aliyepagawa-mtu wa kuogopwa.

## 10. Ujumbe maalum kwa mwalimu

Ni muhimu sana kwa walimu na wafanyikazi kuonyesha mitazamo na hisia za kiungu kwa Wakristo wapya wanapofeli. Tunapaswa kuonyesha wazi huzuni wanapofeli. Mara nyingi tunaonyesha hasira au mtazamo unaoonyesha kuwakataa au kuwalaani wale wanaoshindwa. Mtazamo ambao Yesu alikuwa nao kwa yule mwanamke aliyekamatwa akizini ndio ufaao kwetu kuwaonyesha Wakristo wapya wanaposhindwa. Ita dhambi — dhambi — wala usimhukumu mtu.

## 11. “Acha kujihukumu!” na David Wilkerson

Katika mandharinyuma ya maelezo ya mwalimu yanayofuata mpangilio huu, somo ni uchapishaji kutoka kwa nakala ya David Wilkerson, “*Acha kujihukumu!*” (Tazama kurasa 20-25 katika Mwongozo wa Mwalimu.) Unaweza kutaka mwanafunzi wako mmoja au wote wasome nakala hii. Unaweza pia kuwaambia waandike ripoti na / au waripoti juu ya kile walichojifunza kutoka kwa kifungu hiki.


## 12. Hoja C, Kuelewa shida zangu Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 9-10

Tumia sehemu kubwa ya somo kujadili Hoja C, “*Kuelewa shida zangu.*” Hoja 4 zifuatazo katika mpangilio huu wa somo (#13-16) zinatoa maelezo zaidi juu ya kufundisha sehemu hii ya somo.

Chati iliyo kwenye ukurasa 10 imechukuliwa kutoka semina ya Institute in Basic Life Principles. Ikiwa umewahi kuhudhuria semina hiyo, unaweza kuangalia maelezo yako kutoka kwa sehemu hiyo ya semina unapojiandaa kwa kipindi hiki cha darasa.

## 13. Mfano wa Mwamba wa barafu (dakika 3-5) . . . . . ukurasa wa 9, Mwongozo wa Mwanafunzi

Tanguliza sehemu hii ya somo kwa mfano wa mwamba wa barafu. Tazama mfano katika ukurasa wa 9 wa Mwongozo wa Mwanafunzi. Chora kwenye ubao mstari wa maji ya bahari. Kisha weka sehemu ya mwamba wa barafu iliyo juu ya maji.



Unaweza kutafuta picha ya mwamba wa barafu ili uitumie katika sehemu hii ya somo. Kuna picha nzuri za miamba ya barafu zinazopatikana kwa urahisi kwenye mtandao. Mojawapo ya picha iko kwenye wavuti: [www.iTeenChallenge.org](http://www.iTeenChallenge.org), katika sehemu ya Mtaala wa Mwanafunzi, Mafunzo ya Kikundi cha Wakristo Wapya, Kukua Kwa Kufeli, Vifaa vya kufundisha, Vifaa vya Ziada. Unaweza pia kuipata kwa kutafuta neno “mwamba wa barafu” katika wavuti hiyo.

Unaweza pia kutafuta injini ya utafiti kama Google, na uandike “picha ya mwamba wa barafu” na utapata picha kadhaa. Kujumuisha haya kwenye uwasilisho wa PowerPoint katika darasa lako, kutasaidia kuisitiza hoja kwamba kilicho chini ya maji ni kikubwa zaidi kuliko kilicho juu.

Uliza darasa ni kiasi gani cha mwamba wa barafu kilicho chini ya maji ikilinganishwa na mwamba ulio juu ya maji. Sehemu iliyo chini ya maji ni kubwa mara 9-10 kuliko sehemu iliyo juu ya maji.

Sasa angalia chati kwenye ukurasa wa 10 wa Mwongozo wa Mwanafunzi. Tutatumia barafu hii kuonyesha sehemu nne tofauti za chati hii. Matatizo ya nje ni kama sehemu ya barafu iliyo juu ya maji. Watu wengine wanaweza kuona shida hizi.

## 1

Sehemu ya mwamba wa barafu iliyo chini ya wa maji ni kama sababu za nje za matatizo yetu — mitazamo yako ya ndani. Mifumo hii ya kufikiri, kawaida hututia mashakani. Mitazamo yetu hujidhihirisha kupitia matendo yetu na maneno yetu.

#### 14. Tanguliza chati ya matatizo yetu

(3-5 dakika) . . . . . ukurasa wa 10, Mwongozo wa Mwanafunzi

Waache wanafunzi warudi kwenye ukurasa wa 10 wa Mwongozo wa Mwanafunzi na upitie kwa haraka chati nzima. Onyesha kuwa mifano iliyotolewa katika **matatizo yaliyo juu** na **sababu za kijuujuu** ni mifano michache tu ya haya. Unaweza kuongeza mifano mingine inayohusiana na matatizo na mitazamo ambayo wanafunzi wako wanakabiliwa nayo kwa kawaida.

### Chati ya Matatizo

|  |  |   |  |
|--|--|---|--|
| <b>Matatizo yaliyo juu</b><br>Watu Wengine<br>wanaweza kuona shida hizi      | (Mifano)<br>Kubishana<br>Kupigana<br>Kushutumu<br>Dawa za kulevya<br>Uvutaji sigara  | (Mifano)<br>Kuiba<br>Kusema uwongo<br>Kuwa mbinafsi<br>Kulaani<br>Kulewa        | (Mifano)<br>Dhambi za ngono<br>Kutamani<br>Ushoga<br>Usagaji<br>Uzinzi<br>Kujamiana na jamaa wa ukoo |
| <b>Sababu za Kijuujuu</b><br>Mitazamo ya kindani                             | (Mifano)<br>Uasi<br>Kutoaminiana<br>Kuhisi duni<br>(kuhisi kutokuwa muhimu)  | (Mifano)<br>Hofu<br>Wasiwasi<br>Kutokuwa na usalama<br>Kiburi                   | (Mifano)<br>Kuchanganyikiwa<br>Hofu<br>Hatia<br>Aibu   |
| <b>Matatizo ya Kina</b><br>Msingi<br>Hulka<br>Migogoro<br>Waebrania 12:15-17 | Uchungu<br><br>(Kukasirika au chuki)   | Kuthamini Mali<br>(Kuweka thamani yako katika vitu ambavyo vinaweza kuondolewa) | Uasherati<br>(Dhambi za ngono)   |
| <b>Sababu kuu</b><br>Jibu langu kwa Mungu<br>Isaya 53:6<br>Isaya 55:7        | Kufanya mambo kwa njia yangu badala ya kufanya mambo kwa njia ya Mungu.<br>(Kupinga na kukataa hamu na nguvu unayopewa na Mungu kukabiliana maisha jinsi Anavyotaka niishi.) |   |  |

Chati hii inategemea nyenzo zilizo chukuliwa kutoka kwa daftari ya semina ya *Taasisi ya Kanuni za Msingi za Maisha*.

Waeleze wanafunzi kuwa kuna **Matatizo ya Kina**. Mtazamo wowote au tatizo la juu linaweza kutokana na matatizo matatu makuu. Matatizo haya makuu ni makubwa na ni ya ndani zaidi kuliko mitazamo. Ni matatizo yaliyokita mizizi ambayo humwathiri mtu. Inaweza kuwa na ushawishi mkubwa katika kuamua jinsi mtu atafikiria, atahisi na ataishi.

Unapojadili sababu zingine za juu — mitazamo ambayo iko chini kabisa — eleza kwamba mtazamo unaweza kuwa na “Tatizo kuu” zaidi ya moja. Inaweza kuwa na matatizo mawili makuu au yote matatu yaliyoorodheshwa kwenye chati hii.

**Sababu kuu** cha matatizo yako yote na kufeli yameelezwa katika maelezo yaliyo kwenye chati — “Kufanya mambo kwa njia yangu badala ya kufanya mambo kwa njia ya Mungu.” Maelezo ya pili yaliyotolewa ni njia nyingine ya kusema kitu kimoja, lakini kwa njia ya kiufundi na ya kina zaidi. Unaweza kuashiria umuhimu wa mambo manne tofauti yaliyoorodheshwa katika sentensi hiyo. (1) “Kupinga na (2) kukataa (3) hamu na (4) nguvu unayopewa na Mungu kukabiliana maisha jinsi Anavyotaka niishi.”

### 15. Mifano ya viwango tofauti vya matatizo (dakika 3-5). . . . . ukurasa wa 10, Mwongozo wa Mwanafunzi

Sasa rudi kwenye chati na utoe mifano kadhaa kutoka kwa maisha ambayo huonyesha tatizo kutoka nje hadi kwenye chanzo chake. Unaweza kuelezea umuhimu wa kila hatua kwa tatizo kijumla.

Mwanafunzi mmoja aliondoka kwenye kituo cha Changamoto kwa Vijana baada ya kuwa huko kwa wiki 2-3. Wanafunzi walipoulizwa kwa nini aliondoka, walisema, “Oh, yeye hangeacha kuvuta sigara, hivyo basi akaondoka.” Walifahamu tu tatizo la juu. Ikiwa walitaka kujua ni kwa nini uvutaji sigara ulimshika, basi wangeuliza kuhusu mtazamo wa juu uliosababisha tatizo hili. Kwa bahati mbaya, tatizo la juu la uvutaji sigara linaweza kuwa na sababu nyingi tofauti za juu (mitazamo).

Waambie wanafunzi wachunguze mfano huu kwa undani zaidi. Waambie watafute ni nini kinaweza kuwa sababu za juu na sababu za msingi za tatizo la mtu huyu la kuvuta sigara.

Onyesha kwamba Mungu ana mpango wa kutumia matatizo yetu kama njia ya ukuaji. Tutazungumza juu ya haya kwa undani zaidi katika masomo 3 yafuatayo.

### 16. Mifano ya aina mbalimbali ya matatizo (dakika 3-5). . . . . ukurasa wa 10, Mwongozo wa Mwanafunzi

Hakikisha unatoa mifano kadhaa ya matatizo yanayowaathiri watu. Wakati mwingine, tunaweza kukosa kuona uzito wa tatizo katika maisha ya mtu kwa sababu tunaona tu maswala ya juu.

Dalili ndogo sio ishara ya tatizo ndogo kila wakati. Na dalili kubwa si ishara ya tatizo kubwa kila wakati.

Miaka kadhaa iliyopita mke wangu alikuwa na dalili ya kupoteza kumbukumbu ya muda mfupi mara kwa mara. Wakati mwingine sisi husahau mambo, lakini kwa upande wake ilionekana kuzidi kusahau kwa kawaida. Baada ya kwenda kwa daktari mara kadhaa, mwishowe aliagiza uchunguzi wa MRI kwenye ubongo wake.

## 1

Iligunduliwa kuwa alikuwa na uvimbe wenye ukubwa wa mpira wa gofu chini ya ubongo wake. Upasuaji wa ubongo ulihitajika kuondoa uvimbe huu.

Kupoteza kumbukumbu hokusababishwi na uvimbe wa ubongo kwa kila mtu. Lakini katika mfano huu, dalili ndogo sana ilikuwa dalili ya tatizo kubwa sana kwa mke wangu. (Tangu upasuaji, dalili za kupoteza kumbukumbu zilipotea na amekuwa na afya bora.)

**17. Eleza uhusiano ulioko kati ya aina hizo 4 (dakika 3-5). . . . . ukurasa wa 10, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Inaweza kuwa vyema kurudi kwenye chati na kuelezea kwa undani uhusiano kati ya makundi hayo manne. Itakuwa vyema wakati huu kutumia muda kidogo kuzungumza juu ya njia tofauti za kutatua matatizo haya.

Mfano wa mwamba wa barafu, husaidia kuonyesha matokeo ya kutumia njia tofauti za kutatua matatizo haya. Kwa mfano, ikiwa mtu atatua tatizo la juu, bila kufanya juhudi zozote za kushughulika sehemu zingine tatu, kuna uwezekano kuwa tatizo lili hili la juu au lingine litaibuka hivi karibuni. Ukikata sehemu ya mwamba wa barafu ulio juu ya maji, sehemu nyingine ya barafu haitabaki imezama. 10% ya juu ya mwamba wa barafu itaelea juu ya maji.

**18. Jadili Hoja D. Matokeo ya kufeli (dakika 5-10). . . . . ukurasa wa 10-13, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Eleza kwa kifupi matokeo ya kufeli. Sisitiza kuwa kuna matokeo mazuri na mabaya ya kufeli. Hakikisha kwamba unarudi kwenye aina tatu kuu za kufeli ambazo tulizungumzia mwanzoni mwa somo hili — kufeli ambako sio dhambi, kufeli ambako ni dhambi, na kufeli kunakosababisha dhambi. Matokeo mengi yaliyorodheshwa katika Mwongozo wa Mwanafunzi, yanaonyesha athari wakati kufeli ni dhambi.

Unaweza pia kuwaambia watoe majibu yao kutoka kwa Mwongozo wa Somo zoezi1 ambapo waliorodhesha matokeo mazuri na mabaya ya kufeli.

Tutazungumza zaidi juu ya matokeo ya kufeli katika masomo yaliyosalia ya kozi hii.

**19. Matumizi Binafsi (dakika 5-10)**

Kwa matumizi ya kibinafsi ya somo la leo, kila mwanafunzi afikirie juu ya shida ambazo zinawafanya kufeli kwa sasa.

1. Wacha kila mwanafunzi aandike shida moja ya juu aliyonayo ambayo ananuia kushinda.
2. Waambie waandike wanachofikiria ni sababu ya juu (mtazamo wa ndani) ya tatizo hili.
3. Waambie waandike mojawapo ya matatizo makuu yanayohusiana sana na shida yao

4. Ikiwa wana wakati, labda wanaweza kuandika jinsi sababu kuu inalingana na tatizo hili. Waambie watoe angalau mifano 1 au 2 ya jinsi wamekuwa “wakifanya mambo kwa njia yao,” katika kutatua tatizo hili.
5. Wahimize kuandika njia ya Mungu ya kukabiliana na tatizo hili.

Unaweza kuwaambia waandike kazi hii na wailete kwenye kipindi kijacho cha darasa ikiwa hawana muda wa kuikamilisha darasani.

Ikiwa una muda katika siku nzima, ingekuwa vyema kwako kujadili na kila mwanafunzi majibu waliyotoa kwa zoezi hili. Ikiwa una darasa la *Mafunzo ya Kibinafsi kwa Maisha Mapya* katika kituo chako, unaweza kujadili zoezi hili lilioandikwa na kila mwanafunzi wakati huo.

Usishangae ikiwa watakuwa na wakati mgumu kufahamu vyema sababu ya juu na matatizo makuu yanayohusiana na matatizo yao ya juu. Pia, kunaweza kuwa na mtazamo zaidi ya mmoja wa ndani ambao unahusika katika shida yao.

## 20. Kazi

- A. Sahihisha Mwongozo wa Somo Zoezi la 1, *Kuangalia Kufeli Mara ya Kwanza*.
- B. Eleza Mwongozo wa Somo zoezi la 2 juu ya *Msamaha na Marejesho*. Wanapaswa kukamilisha zoezi hili kwa kipindi kijacho cha darasa.
- C. Waambie wanafunzi wako wasome Sura ya 2 katika Mwongozo wao wa Mwanafunzi ili kujiandaa kujadili katika kipindi kijacho cha darasa.

## 21. Tathmini ya somo

Hebu andika mawazo yako kuhusu jinsi ya kuboresha somo hili.

Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?

Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?

Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

## 1

**Acha kujihukumu!**

Na David Wilkerson

Ninaaibika ninapokumbuka huduma yangu ya hapo awali — kwa sababu niliwahukumu watu wengi wa kweli. Sikuwa na ubaya, na mara nyingi juhudi zangu zilikuwa za kweli na zenye nia nzuri. Lakini ni watu wangapi ambao niliwahukumu kwa kuwa hawakuwa watakatifu kwa mujibu wa mawazo yangu?

Miaka iliyopita nilihubiri dhidi ya kujipodoa kwa wanawake. Nilihubiri dhidi ya nguo fupi. Nililaani kila kitu ambacho hakikuwa “halali” kwenye orodha yangu. Hapo zamani, niliwahi kuhubiri mahubiri makali sana nikilaani mashoga, waliotalikiana, wanywaji pombe na wanaoridhiana. Bado nimeshikilia wazo kwamba wahudumu lazima wazungumze dhidi ya kuingilia dhambi na maridhiano katika maisha ya Wakristo. Bado sipendi kumwona mwanamke ambaye ni Mkristo akionekana kama kahaba. Bado sipendi nguo fupi. Ninaamini, zaidi ya hapo awali, kwamba Mungu anachukia talaka. Bado nimeshikilia wazo kwamba Mungu hatafumbia macho dhambi yoyote au upatanisho wa aina yoyote.

**Lakini hivi karibuni** — Mungu amekuwa akinihimiza kuacha kuwalaani watu ambao wamefeli, na badala yake niwahubirie ujumbe wa upendo na upatanisho. Kwa nini? Kwa sababu kanisa la leo limejawa na Wakristo ambao wamelemewa na hatia na hukumu kubwa. Hawahitaji mahubiri ya habari za hukumu na hofu — tayari wamejawa na hofu ya kutosha na wasiwasi. Hawahitaji kusikia mhubiri akiwaambia jinsi Mungu alivyokasirika nao. Tayari, wana hofu kuu juu ya ghadhabu ya Mungu. Wanahitaji kusikia ujumbe ambao Yohana alihubiri —

**“Kwa maana Mungu hakumtuma Mwanawe ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu; bali ili ulimwengu kupitia yeye uokolewe.” (Yohana 3:17)**

Yesu alimwambia mwanamke mzinzi, “Wala mimi sikuhukumu – Nenda na usitende dhambi tena.” Sasa kwa nini mimi pamoja na makasisi wenzangu, tusihubiri ujumbe huo huo wa upendo kwa maelfu ambao leo wanaishi katika hofu ya uzinzi? Kwa nini bado tunawalaani Wakristo waliotalikiana na wameoa tena — wakati wametubu kwa kweli na wameamua kutotenda dhambi tena kwa njia hiyo?

Hivi karibuni, kijana wa miaka kumi alinisimamisha baada ya mkutano wa injili na kuniomba nisikie hadithi yake. Alikuwa mwenye hamaki. “Mama na Baba yangu waliachana miaka miwili iliyopita. Mama ni Mkristo mzuri, na aliolewa na mwanamume mzuri wa Kikristo. Ninaishi na Mama na baba yangu wa kambo kwa sasa, na ninawapenda sana. Lakini Mama yangu huwa na huzuni kila wakati, na analia sana — kwa sababu kasisi mmoja alimwambia kuwa anaishi katika dhambi. Je! Mama yangu anaenda kuzimu kwa sababu ni mtaliki na ameolewa tena na mtu mwingine ambaye pia ni mtaliki? Nimechanganyikiwa, kwa sababu wote ni Wakristo wazuri.”

Nilimwambia yule kijana kile ninachotaka kuambia ulimwengu wote. “Ikiwa ni mtaliki kwa sababu ya uzinzi wake mwenyewe na akaolewa tena — anaishi katika uzinzi. Mungu anachukia uzinzi. Hata hivyo, ikiwa ametubu, Mungu akamsamehe, na akaanza upya kama Mkristo mchangahaishi katika dhambi ikiwa yuko chini ya damu ya Kristo na amesamehewa. Anaweza kuanza maisha mapya bila hatia wala hukumu. Ikiwa Yesu anasamehe uuaji, wizi, uwongo n.k. — Anasamehe pia uzinzi.”



**Inanishangaza kwamba sisi makasisi tuko tayari kwenda Afrika kuhubiri msamaha kwa “makafiri” — lakini hatuko tayari kuhubiri msamaha na upatanisho kwa Wakristo nyumbani.** Kasisi mmoja alinilalamikia watu waliotalikiana, waliovunjika, na wenye shida katika jukumu lake jipya. Nafikiri, “Ndugu yangu, unapaswa kumshukuru Mungu kwa kukuweka kwenye shamba lenye rutuba. Hao ndio watu wanaohitaji msaada wako zaidi. Wanahitaji mtu wa Mungu kuwaonyesha jinsi ya kuanza upya.”

Mimi niko kwenye ndoa yenye furaha, na Mungu akinisaidia, mimi na Gwen tutakuwa pamoja hadi kifo kitakapotutenganisha, na nachukia talaka kwa dhiti. Lakini, inanisumbua kwamba kanisa liko tayari “kuwafutilia mbali” wale wote ambao wamekosea. Kanisa linatoa faraja na kitulizo kwa wale wote ambao ni “wahasiriwa wasio na hatia.” Mke ambaye alidanganywa. Mume ambaye mkewe alimtoroka. Watoto wote wanaumia katika utengano huu.

Na “Je, wahusika” — wenye dhambi, watu ambao waliwakosea wapendwa wao wasio na hatia? Ikiwa ndoa moja kati ya tatu itaishia kwa talaka, inamaanisha kuwa mamilioni ya wanaume na wake ni “watu wenye hatia.” Siko tayari kuwaachilia wenye hatia. Mwizi ambaye alisamehewa na Kristo pale Kalvari alikuwa na hatia. Alikuwa mhusika — alikuwa *mhalifu*. Lakini, katika dhambi yake alimgeukia Kristo kwa imani. Alisamehewa na kuchukuliwa na Kristo kwa utukufu.

**Na je, mashoga na wasagaji-na walevi?** Je! Kuwahukumu kuna faida yoyote? Hapana! Mara elfu hapana! Kristo hakuja kuwahukumu wenye dhambi, bali kuwaokoa kwa upendo. Mungu huchukia vitendo vya ushoga, lakini hawadharau watu ambao hawaishi kulingana na majukumu ya kiume au ya kike.

Wiki iliyopita, muuguzi mwema wa miaka 19 alinisimamisha baada ya mkutano. Kwa machozi ya kusikitisha alikiri — “Bwana Wilkerson. Mimi ni msagaji. Najisikia mchafu sana. Niliambiwa nisirudi tena kwenye Kanisa ambalo nilikuwa nikienda. Kasisi alisema hangetaka niwadanganye wengine katika kanisa lake. Nahisi kujiua ndio njia pekee. Nina hofu kabisa na hukumu. Lazima niujiue ili nipate amani?”

Aliendelea kusonga mbali nami kana kwamba alikuwa mchafu sana mbele yangu. Nilimuuliza ikiwa bado anampenda Yesu. “Ah, ndio,” alijibu. “Ninapoamka, kila saa moyo wangu humlilia. Nampenda Kristo kwa kila kitu kilicho ndani yangu — lakini nimefungwa na tabia hii mbovu.”

Ilikuwa vyema sana kuona uso wake uking'aa wakati nilipomwambia kuwa Mungu anampenda — hata katika shida zake. Nilimwambia, “Asijiwachilie kwa dhambi zake. Mungu huchora mstari pale ulipo. Hatua yoyote kuelekea kwake inahesabiwa kuwa yenye haki. Kurudi nyuma na kuvuka mstari huo, mbali na Yeye, ni dhambi. Tukisonga karibu naye, Yeye husonga karibu nasi. **Piga hatua yako ya kiroho! Endelea kumpenda Yesu — ingawa bado huna ushindi kamili. Kubali msamaha wake wa kila siku. Ishi siku moja kwa wakati! Amini kuwa Yesu anawapenda wenye dhambi — kwa hivyo lazima akupende wewe pia!**”

Alitabasamu tabasamu la utulivu na kusema, “Bwana Wilkerson, wewe ndiye kasisi wa kwanza kunionyesha mwanga wa matumaini. Ndani ya moyo wangu najua bado Ananipenda — na najua Atanikomboa kutoka kwa minyororo hii. Lakini nimehukumiwa sana na kila mtu. Asante kwa ujumbe wako wa matumaini na upendo.”

## 1

**Msomaji wa ujumbe huu — je! Unaishi sasa chini ya hukumu? Je! Umemkosea Bwana — umemhuzunisha Roho Mtakatifu maishani mwako? Je! Unapigana na jaribu kubwa linalokushinda?**

Unalopaswa kufanya ni kusoma Neno la Mungu na utamfahamu Mungu wa rehema, upendo na huruma isiyo na kikomo. Daudi alisema:

**“BWANA, kama Wewe ungehesabu maovu, Ee Bwana, nani angesimama?  
<sup>4</sup>Lakini kwako kuna msamaha, Ili Wewe uogopwe.” (Zaburi 130:3-4)**

Mwanamke aliyefadhaika alikuja ofisini kwangu akilia, “Bwana Wilkerson, Mungu aliwahi kuniponya kutoka kwa ulevi. Hata hivyo, hivi karibuni nilivunjika moyo na kurudia kunywa pombe. Sasa siwezi kuiwacha pombe. Nimemkosea Bwana vibaya na kile ninachoweza kufanya sasa ni kukata tamaa. Baada ya yale yote Aliyonifanyia mimi, nikifikiria jinsi nilivyo Mkosea. Hamna haja – Sitafanikiwa kamwe.”

Ninaamini kuwa kuna kushindwa kwingi kwa kiroho na wengi wetu hawatambui. Na kuna mkakati wa kiroho wa kufanya kushindwa huku kuwa ukuta ili kuwaweka walioshindwa mbali na Mungu. Hata hivyo, hatupaswi kumwacha shetani kubadilisha kushindwa kwetu kwa muda mfupi kuwa jehanamu ya milele.

Ninaamini kuna mamilioni ya watu kama kijana ambaye ni baharia aliyekuwa kuniona. Kwa machozi alisema, “Baba yangu ni kasisi, lakini nimemkosea sana. Mimi ni dhaifu, nina hofu kuwa kamwe sitamtumikia Bwana inipasavyo. Ninashawishika kutenda dhambi kwa urahisi.”

Kiri kana kwamba haya ni mabaya. Hata hivyo, nimepata faraja kubwa kwa kufahamu kwamba baadhi ya wanaume na wanawake wakuu katika Biblia walifeli na kushindwa.

Je! Ungedhani Musa alifeli? La hasha! Alikuwa kiongozi wa taifa la Israeli kwa zaidi ya miaka 40. Lakini, ukiangalia kwa makini maisha ya mtoa amri, kazi yake ilianza na uuaji, ikifuatwa na miaka arobaini ya kujificha ili haki isitendeke.

Musa alikuwa mtu mwenye woga na asiye na imani. Wakati Mungu alimwita aongoze Waisraeli kutoka utumwani, aliomba, “mimi si msemaji, tokea zamani, wala tokea hapo uliposema na mtumishi wako; maana mimi si mwepesi wa kusema, na ulimi wangu ni mzito.

<sup>13</sup>Akasema, Ee Bwana, nakuomba, tuma kwa mkono wake huyo utakayemtuma.”

(Kutoka 4:10.13). Hili lilimkasirisha Mungu (4:14). Maisha yake yote, Musa alitamani kuingia katika Nchi ya Ahadi, lakini kufeli kwake kulimzuia. Hata hivyo, Mungu Anaulinganisha uaminifu wa Musa na wa Kristo katika Waebrania 3:1, 2.

Kufeli hakukumwondoa Musa kwenye orodha ya mabingwa wa Mungu.

Kwa kawaida, tunamfikiria Yakobo kama shujaa- mkuu wa maombi ambaye alishindana na malaika wa Bwana na kushinda. Yakobo alipewa maono ya mbingu na malaika wakipanda na kushuka. Hata hivyo maisha ya mtu huyu yalijazwa na kufeli kwingi, na maandiko hayajaficha lolote.

**Akiwa kijana, Yakobo alim danganya baba yake aliyekuwa kipofu na kuiba urithi wa kaka yake.** Alipooa, alimdharau mkewe Lea huku akiwa na mapenzi makubwa ya siri kwa dada yake Rachel. Hakukubali jukumu lake kama mume. Baada ya kuzaliwa kwa mtoto wa kiume, Lea aliendelea kusema, “Basi wakati huu mume wangu ataungana nami,” (Mwanzo 29:34). Lakini ukweli ulikuwa — Yakobo alimchukia.

Hapa ni mtu aliyekamatwa kwenye wavuti wa hila, ufisadi, wizi, kutokuwa mwaminifu na kuwaoa mabibi wengi. Walakini, bado tunaabudu Mungu wa Ibrahimu, wa Isaka na wa Yakobo.

Mfalme Daudi, mwimbaji wa zaburi na shujaa hodari, alifurahishwa na sheria ya Bwana na akaonekana kama mtu mwadilifu ambaye hakusimama kati ya wenye dhambi. Hata hivyo, udhaifu wa mtu huyu mkuu unashitua. Alimchukua Bathsheba kutoka kwa mumewe Uria, alimtuma mtu huyo asiye na mashaka afe katika safu ya mbele ya jeshi lake. Nabii Nathani alitangaza dhambi hii maradufu iliyowapa adui za Bwana nafasi kubwa ya kukufuru.

Fikiria mfalme mkuu amesimama karibu na jeneza la mtoto wake haramu aliyekufa, mke aliyeibiwa kando yake na ulimwengu uliojaa maadui waliomlaani Mungu kwa sababu ya dhambi zake mbaya. Daudi anasimama kama mtu aliyefeli kabisa. Hata hivyo, Mungu alimwita Daudi mtu aupendezaye moyo wake (1 Samweli 13:14). Alimbariki Musa na Yakobo mwongo, kwa sababu watu hawa walijifunza jinsi ya kufaidi kutokana na makosa yao na kuendelea na ushindi.

Ikiwa umekatishwa tamaa na kufeli kwako, nina habari njema kwako. Hakuna aliye karibu na Ufalme wa Mungu kuliko mwanamume au mwanamke au kijana ambaye anaangalia kufeli kwa macho yake, akajifunza kuikabili, na kuendelea na maisha ya amani na ushindi. Hapa kuna mpangilio wa kufanya hivyo.

**1. Usiogope kufeli.** Hii inaonekana kama athari ya moja kwa moja. Wakati Adamu alitenda dhambi, alijaribu kujificha kutoka kwa Mungu. Wakati Petro alimkana Kristo, aliogopa kumkabili. Wakati Yona alipokataa kuhubiria Ninawi, hofu yake ilimpeleka baharini ili kukimbia kutoka kwa uso wa Bwana.

Lakini Mungu amenionyesha ukweli ambao umenisaidia mara nyingi: **Kitu kibaya zaidi kuliko kufeli ni hofu inayokujia.** Adamu, Jonah na Petro walimkimbia Mungu sio kwa sababu walikuwa wamepoteza upendo wao kwake, mbali ni kwa sababu waliogopa kuwa amewakasirikia sana Asiweze kuelewa. Shetani hutumia hofu kama hiyo ili kuwafanya watu wafikirie kuwa hamna haja ya kujaribu.

“Mshtaki wa ndugu” wa zamani anasubiri kama tai- mzoga ili ufeli kwa njia fulani. Kisha anatumia kila uwongo kuzimu kukufanya ukate tamaa, kukufanya uamini kwamba Mungu ni mtakatifu sana au wewe ni mwenye dhambi kiasi kwamba huwezi kurudi. Au anakufanya uogope kuwa haujakamilika vya kutosha, au anakuambia kuwa hautaweza kushinda kufeli kwako.

Ilichukua miaka arobaini kuondoa hofu ya Musa na kumfanya wa kutumika katika mpango Mungu. Wakati huo, mpango wa Mungu wa ukombozi ulicheleweshwa kwa takriban nusu karne wakati mtu mmoja akijifunza jinsi ya kukabiliana na kufeli. Ikiwa Musa au Yakobo au Daudi wangejisalimisha kwa kufeli, labda hatungewahi kusikia juu ya watu hawa tena. Hata hivyo, Musa aliinuka tena kuwa mmoja wa mashujaa wa Mungu. Jacob alikumbana na dhambi zake, alipokutana tena na kaka ambaye alikuwa amedanganya, alifikia kiwango kipya cha ushindi. Daudi alikimbia katika nyumba ya Mungu, akashika pembe za madhabahu, akapata msamaha na amani na kurudi kwenya saa bora. Yona alirudia hatua zake, akafanya kile alichokuwa amekataa kufanya mwanzoni na kuleta jiji lote – katika hali ya toba na ukombozi. Petro aliinuka kutoka kwenye majivu ya kukataa na kuliongoza kanisa kwenye Pentekoste.

## 1

**2. Licha ya kufeli, endelea kusonga mbele.** Kila baada ya kushindwa, ndipo mtu hufanya kazi yake kubwa kwa Mungu. Miaka ishirini iliyopita niliketi kwenye gari langu dogo, nikilia — Nilifeli vibaya, nilifikiri. Nilikuwa nimefurushwa nje ya korti baada ya kufikiria niliongozwa na Mungu kushuhudia mauaji saba ya vijana wauaji. Niliona picha yangu kwenye magazeti ya udaku yenye mada, “MHUBIRI ANAYEBEBA BIBLIA KUKATIZA KESI YA MAUAJI.” Jaribio langu la kumtii Mungu na kuwasaidia vijana hao lilionekana kuishia kwa kufeli.

Ninatetemeka kufikiria baraka ambazo ningekosa ikiwa ningekata tamaa wakati ule wa giza. Nina furaha leo kwa kuwa Mungu alinifundisha jinsi ya kukabiliana na kufeli kwangu na kuchukua hatua yake ya kwa ajili yangu.

Ninawajua watu wawili mashuhuri wa Mungu — ambao waliwahudumia maelfu ya watu-ambao walianguka katika dhambi ambayo Daudi alifanya na Bathsheba. Kasisi mmoja aliamua kwamba hawezi kuendelea. Leo, anakunywa pombe na kumlaani Kristo aliyewahi kuhubiri juu yake. Mtu huyo mwingine alitubu na kuanza upya. Sasa anaongoza programu ya umisheni ya kimataifa inayowafikia maelfu kwa Kristo. Kushindwa kwake kumeachwa nyuma. Anaendelea kusonga mbele.

Katika kazi yangu na walevi wa dawa za kulevyu na wale ambao hawawezi kubadilika, nimeona kwamba wengi wa wale wanaorudi kwenye tabia zao za zamani wanakuwa na nguvu kuliko wengine wote wanapokabiliwa na kufeli kwao na kurudi kwa Bwana. Wana ufahamu maalum wa nguvu za Shetani, jumla, kukataa imani katika mwili.

**3. Pamoja na kushindwa, endelea kuabudu.** Kulikuwa na njia moja tu ya Musa kuishi kwa ushindi, kwa sababu alikuwa na tabia kama wengi wetu leo. Aliendelea kushirikiana na Bwana, “... ana kwa ana, kama mtu anavyozungumza na rafiki yake” (Kutoka 33:11). Musa alidumisha urafiki huo wa karibu na Mungu. Ninaamini siri ya utakatifu ni rahisi sana: Kaa karibu na Yesu. Endelea kumtazama usoni hadi uwe kama unavyomwona.

Jioni moja mwanamke mkorofi alinisimamisha barabarani na akakiri mambo mabaya. Akishika mkono wangu kwa nguvu sana nilifikiri atauharibu, akasema, “Bwana Wilkerson, ninakabiliwa na wakati mbaya zaidi maishani mwangu. Sijui nifuate njia gani. Mume wangu aliniacha na yote ni makosa yangu. Ninapofikiria jinsi nilivyomkosea Mungu na familia yangu, ninakosa usingizi usiku kucha. Je, Nitafanya nini?”

Niliguswa kumwambia, “Rafiki yangu, inua mikono yako, hivi sasa kwenye kona hii ya barabara, na uanze kumwabudu Bwana. Mwambie unajua kwamba umefeli, lakini bado unampenda hivyo. Kisha nenda nyumbani upige magoti. Usimwombe Mungu lolote- inua moyo wako na mikono yako, na umwabudu.”

Nilimwacha yule mwanamke akiwa amesimama kwenye kona ya barabara huku mikono yake ikiwa imeinuliwa juu, machozi yakitiririka mashavuni mwake, akimsifu Bwana na tayari akionja ushindi ambao ulikuwa umeanza kurejea maishani mwake.

Sasa, wacha nizungumze juu ya kufeli kwako. Je, kuna shida nyumbani kwako? Je, baadhi ya tabia zinazodharauliwa zimedhibiti maisha yako kiasi kwamba huwezi kuwa huru? Je, unateswa akilini au rohoni? Je, Mungu amekuambia ufanye kitu ambacho umeshindwa kufanya? Je, uko nje ya mapenzi ya Mungu? Je, unavutiwa na kumbukumbu ya maisha yako ya zamani? Au kwa maono ya kile unaweza kuwa?

**Kisha mwabudu Bwana katikati ya kushindwa kwako! Msifuni! Mtukuze!**

Yote haya yanaweza kusikika kama yamerahisishwa kupita kiasi, lakini njia tu ya kukabiliana na kufeli na kufanikiwa ni rahisi kwa watoto na watu wazima. Kristo anasema,

**Yeyote ajaye kwangu sitamtupa nje. (Yohana 6:37)**

**Njooi kwangu, nyinyi nyote (mlioshindwa) wenye mizigo mizito,  
nami nitawapumzisha. (Mathayo 11:28)**

Usiwe na hofu ya kushindwa. Endelea licha ya hayo. Mwabudu Mungu mpaka ushindi utakapokuja. Sehemu ngumu zaidi ya imani, ni saa za mwisho. Endelea, na utakabiliwa na saa yako nzuri zaidi.

## Somo la 2

### Hatua za kwanza za kupona kutokana na kufeli

# 2

#### 1. Kweli kuu ya Kibiblia

Ninahitaji msaada wa Mungu kuchukua hatua zifaazo za kupona kutokana na kufeli.

#### 2. Mstari Mkuu: Zaburi 32:8-9 Bibilia Takatifu (SUV)

<sup>8</sup>Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiondea; Nitakushauri, jicho langu likikutazama.

<sup>9</sup>Msiwe kama farasi wala nyumbu, Walio hawana akili. Kwa matandiko ya lijamu na hatamu Sharti kuwazuia hao, au hawatakukaribia.

#### 3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili

Sura ya 2 katika Mwongozo wa Mwanafunzi inaenda pamoja na somo hili. Zoezi la 2 kwenye Mwongozo wa Somo, “*Msamaha na Marejesho*” linaendana na somo hili.

#### 4. Malipo — maandalizi ya mwalimu

Kurasa 25-28 katika Mwongozo wa Mwanafunzi zinashughulikia suala la ukombozi. Unaweza kutumia kipindi chote cha darasa kujadili mada hii, kulingana na jinsi wanafunzi wako wanavyovutiwa na sehemu hii. Ikiwa idadi kubwa ya wanafunzi wako sio Wakristo, au ni Wakristo wapya sana, unaweza kusoma mada hii kwa ufupi sana na kisha uizungumzie kwa undani zaidi baadaye. Suala la ukombozi linaweza kuwa lenye utata mwingi, na kwa Wakristo wengine wapya suala hilo ni kubwa kwao.

#### 5. Zoezi la utangulizi wa somo (dakika 3-5)

Anza somo la leo kwa kutumia mfano wa mwamba wa barafu kupitia hoja nne zilizo kwenye chati ya “*Kuelewa matatizo yako.*” Tazama ukurasa wa 9-10 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

Pia pitia aina tatu kuu za kutofaulu:

1. Kufeli ambako sio dhambi
2. Kufeli ambako ni dhambi
3. Kufeli ambako husababisha dhambi.

**6. Tanguliza hoja ya kupona na kurudia  
(dakika 2-3). . . . . ukurasa wa 14-15, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Unapoanza majadiliano ya leo, Anza kwa kueleza kwa kifupi dhana za kupona na kurudia ambazo tutatumia katika kozi hii. Katika kurasa za 14-15 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi, kuna maelezo ya kina ya maneno haya mawili. Jambo muhimu kwako ni kuzingatia historia ya wanafunzi wako. Dhana hizi zinaweza kuwa zinafahamika na wanafunzi wako, kulingana na historia yao.

Suala muhimu la kusisitiza hapa ni kwamba tutatumia mtindo wa Kibiblia kukabiliana na kufeli, kupona na kurudia.

**7. Jadili Hoja A. Njia za kawaida za kukabiliana na kufeli  
(dakika 5-7). . . . . ukurasa wa 15-16, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Waambie wanafunzi waandike orodha ya njia tofauti walizotumia kukabiliana na kufeli hapo awali.

Unaweza pia kutumia mwamba wa barafu kueleza njia tofauti za kukabiliana na kufeli. Njia zingine za kawaida zimeelezwa katika Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 15-16.

**8. Jadili Hoja B. Nifanyeje nikifeli?  
(Dakika 10-15) . . . . . ukurasa wa 16-21, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Waeleze wanafunzi kwamba hatua 9 zilizotolewa kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi, ni muundo wa jumla wa kukabiliana na kufeli. Tutaangalia kwa makini baadhi ya masuala, baadaye katika somo la leo (msamaha na ukombozi, kwa mfano), au baadaye katika kozi hii.

**Nifanye nini wakati ninapofeli?**

1. Ninapaswa kukubali kwamba nilikuwa nimekosea
2. Ninapaswa kumwomba Mungu anisamehe
3. Lazima nijisamehe
4. Lazima nifanye uamuzi wa kuacha kutenda dhambi
5. Omba msamaha kwa wale waliokerwa
6. Tafuta kisababishi cha kufeli kwako
7. Tatafuta njia ya Mungu ya kujiondoa kutoka kwa kufeli
8. Wape wengine nafasi wakuambie shida zako
9. Endelea kukua!

*Kukua Kupitia Kufeli Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa 16-21*



## 2

Hakikisha kuwa, katika somo hili unatumia dhana ya “kupona” unapozungumza juu ya kukabiliana na kufeli. Je! hatua za kupona ni zipi? Tunataka wakubali kuwa wanahitaji kupona ili kuangazia watakavyokabiliana na kufeli.

Jambo moja tunalopaswa kuwaambia wanafunzi leo ni kuwa, kupona kutoka kwa kufeli ni mchakato. Makosa madogo yanahitaji hatua ndogo za kupona. Makosa makubwa yanahitaji hatua kubwa za mabadiliko kwa urejesho wa kweli.

Katika somo hili, tunataka kusisitiza kuwa kufeli kunaweza kuwa hatua ya ukuaji ikiwa tutafanya maamuzi yafaayo kuhusu jinsi ya kukabiliana na kufeli.

Katika kujadili hoja ya 3, “Lazima nijisamehe,” onyesha kuwa kuna watu wasiopungua watatu wanaohusika katika hatua hii.

**Kwanza**, ninapaswa kumwomba Mungu msamaha. Mungu atanisamehe. Lakini siwezi kuachia hapo.

**Pili**, ninapaswa kumwomba msamaha mtu aliyeathiriwa na kufeli kwangu. Anaweza kuwa zaidi ya mtu mmoja.

**Tatu**, kuna mtu wa tatu anayehusika katika mchakato huu wa msamaha-wewe mwenyewe. Unahitaji kujisamehe mwenyewe kwa kufeli. Kwa watu wengine, hii ndiyo sehemu ngumu zaidi katika suala zima.

Jadili kwa kifupi hoja ya 5, “Omba msamaha kwa wale waliokerwa,” kwa wakati huu. Eleza kwamba tutashughulikia swala hili kwa undani zaidi baadaye katika somo hili.

## 9. Jadili hadithi za kibiblia za kufeli (dakika 5-15)

Unaweza kuangazia hadithi moja au mbili kutoka kwa Biblia kwa wakati huu, ambazo zinaonyesha jinsi watu wengine walivyokabiliana na kufeli kwao. Unaweza pia kuangalia matokeo ya kufeli kwao. Majadiliano mafupi ya baadhi ya maswala haya yanaweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa vizuri hatua ulizoorodhesha, “Unapaswa kufanya nini unapofeli?”

Hapa kuna hadithi kadhaa za Biblia ambazo zinaweza kutumika hapa.

1. Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni, Mwanzo 3
2. Mgogoro kati ya Kaini na Mungu na ndugu yake, Mwanzo 4:1-16.
3. Mfalme Sauli alipojaribu kuficha kufeli kwake, 1 Samweli 15
4. Dhambi ya Daudi na Bathsheba, 2 Samweli 11 & 12  
(Kumbuka alivyofanya haswa Daudi wakati nabii alipomkabili kwa dhambi yaki. 2 Samweli 12:13-23)
5. Petro alipomkana Kristo, Mathayo 26
6. Mwana Mpotevu, Luka 15:11-32

**10. Tanguliza Hoja C. Kuomba msamaha  
(dakika 2-3) . . . . . ukurasa wa 21-24, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Tanguliza sehemu kuu ya kipindi inayohusika na msamaha. Inaweza kuwa vyema kuwasilisha hoja hii kama hatua moja kwenye mchakato wa kupona. Baada ya kuzungumzia msamaha, tutazungumzia ukombozi. Hata hivyo, inaweza kuwa vyema kusema kuwa msamaha ni hatua moja muhimu katika ukombozi.

Ukombozi ni nini? Ni kurejesha kitu — kukirudisha katika hali ya utendaji. Tunataka kurejesha uhusiano, kurejesha mitazamo na tabia za mafanikio. Tunataka kuona ukuaji mzuri utakaotoka kwa msamaha na urejesho.

Unapojadili msamaha, eleza kwanza umuhimu wa kwenda kwa mtu uliyemkosea kwa kufeli kwako. Eleza kwamba shetani atajaribu kukushawishi kusahau kwenda kwa mtu huyo kumwomba msamaha. Atajaribu kuweka visingizio vya kila aina kichwani mwako vya kwa nini haupaswi kwenda kwa mtu huyo.

Jaribu kufafanua hali zitakazokuwa bora kwa kumwomba mtu huyo msamaha. Kuna kufeli ambako hakumhusishi mtu yeyote isipokuwa wewe mwenyewe na Mungu. Kwa mfano, mtu anaweza kuanguka kwenye jaribu la tamaa, na akilini mwake anafikiria mawazo maovu. Mwenzake pengine hafahamu nini kinaendelea akilini mwake, na kwa hivyo, hakuna haja ya yule aliyefeli kwenda kumwomba msamaha kwa mawazo yake ya tamaa. Kwa kweli, katika hali kama hii, anaweza kufanya maovu zaidi kwa kumwambia mwanzake kuhusu kufeli kwake.

**11. Jadili hoja ndogo 1. Kabla ya kuomba msamaha  
(dakika 5) . . . . . ukurasa wa 21-22, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Jadili mambo wanayopaswa kufanya kabla ya kwenda kwa mtu na kumwomba msamaha kwa yale waliyoyafanya.

- a. Kukubali kwangu mimi na kwa Mungu kwamba nilikosa.
- b. Kufahamu vyema ni nini nilichokosea.
- c. Kupanga nitakachosema nitakapozungumza na mtu huyu.

Hadithi ya Mwana Mpotevu katika Luka 15, inatoa mfano mzuri wa mchakato wa kufuata unapoomba msamaha. Mwana alitambua dhambi yake, akaamua kurudi nyumbani, na akapanga nini atakachosema akifika huko. Unaweza kutumia hadithi hii katika sehemu hii ya somo kuonyesha mambo fulani kuhusu msamaha, na jinsi wahusika watatu wakuu katika hadithi hii wanavyohusika.

Angalia maswali kwenye Zoezi la Pili, katika Mwongozo wa Somo, yanayohusiana na hadithi hii. Unaweza kumwambia mwanafunzi mmoja atoe muhtasari wa hadithi hiyo kwa faida ya darasa zima, kisha watoe majibu yao kwa maswali yanayohusiana.

## 2

**12. Jadili Hoja 2. Njia mbaya za kuomba msamaha na Hoja 3. Njia sahihi ya kuomba msamaha (dakika 5-15) . . . . . ukurasa wa 22-24, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Katika kujadili sehemu hii ya somo, unaweza kuwaambia wanafunzi waigize njia tofauti zisizofaa za kuomba msamaha na njia bora za kuomba msamaha. Wanafunzi wawili wawili waigize mojawapo ya njia za kuomba msamaha.

Ikiwezekana, rekodi video ya maigizo haya. Wanafunzi watapenda kutazama tena, na kila wakati watakapotazama, mafundisho ya sehemu hii ya somo yataimarishwa mioyoni mwao.

Unaporudia tena njia bora ya kuomba msamaha, hakikisha wameelewa sehemu hizi mbili. Sehemu ya kwanza ni kukiri makosa. Wahimize kutambua mtazamo wa ndani (sababu ya juu) na sababu kuu ya kosa, sio tu kosa la juu.

Sehemu ya pili ni kuuliza swali, “Je! Utanisamehe?” Hili linapaswa kutamkwa kama swali. Mara tu wanapouliza swali hili, wanapaswa kusubiri mtu mwingine ajibu.

Jaribu kutoa mifano kadhaa ya jinsi watu wamefanya hivi kwa njia nzuri na matokeo yanakuwa yepi. Unaweza pia kutoa mifano ya watu waliotumia njia zisizofaa kuomba msamaha na matokeo yake.

Sehemu hii yote ya kuomba msamaha na kupata dhamiri safi imejadiliwa kwa undani zaidi katika nyenzo zilizotolewa na *Institute of Basic Life Principles*. Ikiwa umehudhuria semina hiyo, unaweza kuangalia maelezo uliyoyaandika katika semina. Hoja inayowasilishwa katika Mwongozo wa Mwanafunzi kuhusu mada ya msamaha ni sawa na ile iliyotolewa katika semina hiyo.

Unaweza kutaja baadhi ya visingizio vinavyotolewa vya kwa nini njia hii ya kuomba msamaha haifanyi kazi kwa watu wengine. Hivyo ni visingizio tu. Ikiwa njia hii inatumiwa kwa usahihi, inafanya kazi kweli. Ni vyema kwao kujifunza kutokana na kufeli kwao.

**13. Kusamehe na kusahau (dakika 2-5)**

Tatizo kuu kwa Wakristo wengine wanya ni kupata usawa katika kusamehe na kusahau. Wakati mwingine, watu hupenda kusahau juu ya kufeli kwao kabla hawajapata msamaha kwa kile walichokosea. Wanataka pia kusahau juu ya kufeli badala ya kufanya kazi ngumu ya mabadiliko ambayo inahitajika katika sehemu hiyo ya maisha yao.

Hapa ni mtu ambaye anasahau kwa haraka sana kufeli kwake kwa zamani. Wakati mwingine, anasahau kufeli kwake kabla ya kuomba radhi na kuomba msamaha kwa mtu aliyemkosea kupitia kufeli kwake.

Katika hali hiyo, mtu aliyekosewa anaweza kuendelea kuhisi uchungu wa uhusiano uliovonjika. Madhara mengine ya kusahau kwa haraka kufeli, ni kuwa mtu hajifunzi yale yote ambayo Mungu anataka ajifunze kutokana na kufeli. Kwa sababu hiyo, haichukui muda mrefu sana kabla ya mtu huyo kufeli tena katika sehemu moja, kwa sababu hakujifundisha njia ya Mungu ya kuzuia kufeli maishani mwake.

Upande mwingine, ni mtu ambaye hujikumbusha kufeli kwake akilini mwake. Jambo hili huimarisha mtazamo wa ndani, “Nimefeli kabisa.” Mtu huyu anahitaji kutiwa moyo kusema ukweli kuhusu kufeli kwake, kisha kuendelea kuona mambo mazuri yanayotokea maishani mwake.

**14. Maswali kutoka kwa Mwongozo wa Somo Zoezi 2 (dakika 3-5)**

Swali la 6 kwenye Zoezi la 2 linawapa wanafunzi nafasi ya kuandika maswali yoyote waliyonayo juu ya msamaha na urejesho. Unaweza kuchukua wakati hapa kujadili maswali yoyote waliyo nayo juu ya msamaha. Waulize washikilie maswali yao juu ya ukombozi hadi baadaye kwenye kipindi cha darasa wakati utakapojadili suala hili kwa undani zaidi.

**15. Wasamehe wale wanaokukosea (dakika 5)**

Katika majadiliano ya msamaha, lengo kuu ni jinsi ya kuomba msamaha kwa njia inayofaa baada ya kumkosea mtu. Unaweza kutaja kwa kifupi sababu wa kusamehe kwa urahisi wakati mtu anakuja na kukiri kufeli kwake.

**Mithali 17:9 Biblia Takatifu (SUV)**

**Afunikaye kosa hutafuta kupendwa; Bali yeye akashifuye neno hutenga rafiki.**

Suala hili la kuwasamehe wengine ambao wamekukosea ni suala kuu linalopaswa kuzungumziwa katika somo tofauti.

**16. Urejesho — mipangilio ya mwalimu**

Mada ya urejesho pengine inafaa kwenye kategoria ya “nyama”, badala ya kategoria ya “maziwa” kwa chakula cha kiroho. Kwa kuzingatia haya, panga kwa uangalifu jinsi utakavyofundisha somo hili kwa wanafunzi wako. Unaweza kufundisha kwa kifupi baadhi ya masuala ya kimsingi kuhusiana na ukombozi, ukilenga tu baraka zinazokuja baada ya kufuata njia za Mungu.

**17. Tanguliza Hoja D. Kufanya marejesho (dakika 2-5) . . . . . ukurasa wa 25-28, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Wakati unapoelezea pointi hii, hakikisha unaelezea vyema tofauti kati ya kuomba mshamaha kwa kile ilichokosea na kurejesha uhusiano uliovunjika. Jambo hili limeshughulikiwa katika Mwongozo wa Mwanafunzi katika aya ambayo ipo kabla tu ya D. *Kufanya marejesho*.

Hakikisha umelezea kwamba kuomba msamaha kwatakiwa kufanyika haraka iwezekanavyo. Lakini kurejesha uhusiano uliovunjika na kufanya mapatano, ikiwa inahitajika, huenda ikachukua muda mrefu.

Tanguliza mada ya urejesho na ushuhuda wa baadhi ya Wakristo ambao wamefuata mtindo huu wa Kibiblia. Wanafunzi wako wanapaswa kuona mara moja kuwa hii ni sehemu halisi ya maisha ya Kikristo. Usiogope kutumia mifano ya pale ambapo matokeo yalikuwa yenye uchungu. Mifano yako yote sio lazima iwe ya “hadithi za miujiza” ambapo Mungu alifanya kila kitu kiwe kikamilifu. Mfano wa Brian Swails unapatikana kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi kwenye kurasa 26-27.

**18. Jadili Hoja ndogo 1. Mfano wa kibiblia wa urejesho  
(dakika 2-5) . . . . . ukurasa wa 25-27, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Unapowasilisha muundo wa kibiblia wa urejesho, jaribu kuelezea mtazamo wa matarajio mazuri — Mungu anaweza kubadilisha kufeli kuwa kitu kizuri ikiwa tutafuata njia zake. Jadiliana na wanafunzi juu ya maandiko yaliyoorodheshwa kwenye ukurasa wa 25 wa Mwongozo wa Mwanafunzi.

Mathayo 5:23-24

Luka 19:1-10

Wagalatia 6:1-2

Unaweza kurudi kwenye sheria za Agano la Kale na uchunguze kwa ufupi baadhi ya maelezo kuhusu urejesho wakati huo.

**19. Jadili Hoja ndogo 2. Hatua za urejesho  
(5-7 dakika) . . . . . ukurasa wa 27, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Katika kujadili sehemu hii, fafanua mambo yanayopaswa kupewa kipaumbele katika urejesho:

- a. Rejesha uhusiano wako na Mungu kwanza.
- b. Rejesha uhusiano wako na mtu uliyemkosea.
- c. Rejesha kile ulichoiba au kuharibu.

Hadithi ya Zakayo katika Luka 19:1-10, ni mfano mzuri wa jinsi urejesho unavyofaa katika maisha ya Mkristo mpya. Hadithi hii pia inasisitiza jinsi Mkristo mpya anavyofanya urejesho kutoka kwa dhambi zake za zamani, ndivyo itakavyokuwa bora zaidi. Tazama Zoezi 2 kwa maswali unayoweza kutumia katika majadiliano darasani wakati huu.

**20. Usiwalazimisha wanafunzi wako kukubaliana na mafundisho hayo**

Usijaribu kulazimisha wazo hili la ukombozi kwa wanafunzi wako, haswa Wakristo wapya. Tumia mtazamo wa “Wacha tuone nini Mungu anasema kuhusu sehemu hii ngumu ya maisha yetu.” Mwache Roho Mtakatifu awashawishi ikiwa wanahitaji urejesho katika maisha yao wenyewe.

Unaweza kutumia hadithi ya Brian Swails katika Mwongozo wa Mwanafunzi, kurasa 26-27, kama njia ya kuonyesha faida zilizotokana na matendo yake.

**21. Jadili Hoja 3. Matokeo ya kufanya marejesho  
(dakika 3-10) . . . . . ukurasa wa 27-28, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Jadili matokeo ya kufuata mpango wa Mungu wa kufanya urejesho. Taja kwamba Ibilisi atajaribu kuweka hofu ndani ya mioyo yao kama njia ya kuwavunja mioyo ili wasifanye urejesho.

**22. Faida ya Urejesho kwa tabia (dakika 3-5)**

Urejesho mara nyingi sio jambo rahisi, linahitaji ujasiri wa kufuata muundo wa Mungu. Hali hii pia ni fursa kwa Mkristo mpya kukuza sifa nzuri za ndani. Jadili sifa tofauti ambazo wanaweza kukuza katika hali kama hizi.

**23. Kukubali kuwajibika kwa matendo ya zamani (dakika 2-5)**

Suala la ukombozi linahusika moja kwa moja na kuwajibika kibinafsi kwa matendo yako ya zamani. Huu ni udhaifu wa kawaida kwa Wakristo wapya, haswa wale wanaokuja kwenye Changamoto kwa Vijana na huduma sawiya za Kikristo. Hawajajifunza kuwajibika kwa matendo yao ya zamani.

Kanuni ya Kibiblia ya “kupanda na kuvuna” inafaa hapa. Tazama Wagalatia 6:7-8. Kuna matokeo ambayo tutavuna tutakapofeli, tutakapotenda dhambi. Tuna imani kwamba Mungu atasamehe dhambi zetu tutakapokiri kwake. Hata hivyo, msamaha Wake haumaanishi kwamba atafuta kanuni ya kupanda na kuvuna moja kwa moja. Mungu atasamehe dhambi, aondoe hatia, na arejeshe uhusiano na amani ya ndani. Hivi ndivyo ilivyokuwa katika maisha ya Daudi baada ya kukiri dhambi yake ya uzinzi na mauaji. (Tazama 2 Samweli 11 & 12) Matokeo ya dhambi yake yalibaki (2 Samweli 12:14); dhambi zake ziliwapa mataifa yaliyowazunguka nafasi ya kumtukana Mungu.

Mara nyingi kushindwa kwetu kutaacha makovu ya kudumu. Lakini mtazamo wetu dhidi ya makovu haya, unaweza kuwa bora zaidi ikiwa tutafuata muundo wa Mungu wa urejesho na kumruhusu kuleta uponyaji katika mahusiano yaliyoadhirika.

**24. Matumizi binafsi (dakika 5-10)****A. Hatua za kwanza za kupona kutokana na kufeli**

Waambie wanafunzi wako warudi kwenye kurasa za 16-21 katika Mwongozo wa Mwanafunzi na upitie hatua za kwanza ambazo wanapaswa kuchukua wanapofeli. Waambie wataje kufeli ambako bado wanahitaji kushughulikia maishani mwao, na kisha uchague hatua moja au mbili kati ya hizi ambazo wanapaswa kutumia kwa kufeli huko.

**B. Kuomba msamaha**

Wahimize wanafunzi kutumia njia zifaazo za kuomba msamaha. Waache wakariri mtindo rahisi uliotolewa katika Mwongozo wa Mwanafunzi kwenye ukurasa wa 24.

“Nilikosea (*sema ni nini umekosea*). Utanisamehe?”

Unaweza kuwapa dakika kadhaa na uombe. Omba Mungu awafunulie ikiwa wanahitaji kwenda kumwomba msamaha mtu yeyote.

Waambie waandike kile wanachopanga kumwambia mtu huyu. Unaweza kuwaambia waandike ripoti ya kilichotokea walipoenda kumwomba msamaha mtu huyu.

**C. Kufanya urejesho**

Ikiwa una kipindi tofauti cha darasa cha kufanya urejesho utahitaji kuzingatia matumizi ya kibinafsi ya jinsi wanavyoweza kuanza kutumia muundo huu wa Kibiblia katika maisha yao wenyewe. Baadhi ya nyenzo kutoka Semina ya *Taasisi ya Misingi ya Maisha ya Msingi*, zina maoni yanayosaidia sana juu ya jinsi ya kutekeleza mafundisho hayo ya Kibiblia kwa vitendo.

**2****25. Kazi**

- A. Sahihisha Mwongozo wa Somo Zoezi la 2, *Msamaha na Marejesho*, mwishoni mwa darasa.
- B. Wape kazi kutoka kwa Mathayo 6:14-15 mwishoni mwa kipindi cha darasa.
- C. Waambie wanafunzi wako wasome Sura ya 3 katika Mwongozo wao wa Mwanafunzi ili kujiandaa kuijadili katika kipindi kijacho cha darasa.

**26. Tathmini ya somo**

Hebu andika mawazo yako kuhusu jinsi ya kuboresha somo hili.

Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?

Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?

Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?



## Somo la 3

# Jinsi ya kukua kupitia kufeli kwangu

### 1. Kweli Kuu ya Kibiblia

Ninapaswa kumsikiliza na kumtii Roho Mtakatifu ili Anisaidie kukua kupitia kufeli kwangu.

### 2. Mstari Mkuu: Yohana 16:13 Bibilia Takatifu (SUV)

Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.

### 3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili

Sura ya 3 katika Mwongozo wa Mwanafunzi inaendana na somo hili. Zoezi la 3 kwenye Mwongozo wa Somo, *Kufeli Kwangu*, linaenda sambamba na somo hili.

### 4. Zoezi la utangulizi wa somo (dakika 3-5)

Tumia bunduki kuanzisha somo la leo. Kusudi kuu la mfano huu ni kuonyesha sehemu tofauti za matatizo. Tunapofahamu sehemu tofauti zinazohusika, inatusaidia kuona ni jinsi gani tunaweza kujifunza kutokana na kufeli kwetu.

Matayarisho: Chora vielelezo vifuatavyo na maandishi yanayoambatana kwenye PowerPoint au kwenye bango.

#### 1. Mchoro: Bunduki

Maandishi: Bunduki hii ina risasi.

#### 2. Mchoro: Onyesha wingu la moshi linalotoka kwenye pipa la bunduki na mtu anayepigwa na risasi.

Maandishi: Mtu huyu amepigwa risasi.

#### 3. Mchoro: Mtu aliyelala chini.

Maandishi: Mtu huyu amefariki.

#### 4. Mchoro: Onyesha bunduki tena.

Maandishi: Ni nani aliyefyatua risasi?

#### 5. Mchoro: Onyesha mtu mwingine.

Maandishi: Mtu huyu alimpiga risasi.

#### 6. Mchoro & Maandishi: Kwa herufi kubwa weka swali hili. "Mtu huyu ataadhibiwa vipi?"

7. Mchoro: Onyesha mtu mwenye hatia.

Maandishi: Tunawezaje kumsaidia mtu huyu?

Tanguliza Jambo litakalojadiliwa kwenye somo. Sura ya mwisho inaishia kwa swali. Usichukue muda mwingi kujadili kwa kina adhabu itakayofaa. Onyesha kuwa kusudi la somo hili ni kuangalia mambo tofauti yanayohusiana na kufeli.

1. Kuna **hatua ya (kufeli)**: Alifyatua risasi
2. **Matokeo** ya matendo (matokeo), Mtu alifariki.
3. **Sababu** ya kufeli: risasi ilifyatuliwa na mtu. Mtu huyo ndiye sababu halisi ya kufeli, sio bunduki. Alifanya uamuzi wa kuifyatua.
4. **Adhabu au nidhamu** wakati mwingine ni mojawapo ya matokeo ya kufeli. Adhabu hiyo sio sawa na matokeo ya matendo hayo. Matokeo yalikuwa kifo cha mtu mwingine. Adhabu hutolewa kwa sababu ya kufeli.
5. **Suluhu**: Je, mtu anaweza kusaidiwa anapofeli? Tunawezaje kumsaidia mtu huyu aliyefeli kukua?

### 5. Kutanguliza mada ya darasa la leo kwa majadiliano

Katika kipindi cha darasa la leo tutaangazia mchakato wa ukuaji unaohitajika kushinda kufeli na matatizo katika maisha yetu. Tutagawanya haya katika hatua tatu kuu za ukuaji.

- A. Kuyashinda matatizo
- B. Ishi maisha yenye afya
- C. Chukua hatua za kuzuia kufeli tena

Kila moja ya hatua hizi za ukuaji ni muhimu, kwa hivyo, panga muda wako kwa makini ili uweze kushughulikia hatua zote tatu.

Unapaswa kuwakumbusha tena kuwa kufeli kote kunafaa. Kama tulivyojadili katika sura ya 1, tunaweza kugawanya kufeli katika vikundi vitatu vikuu. Katika majadiliano yetu leo, tutaangazia kufeli ambako ni dhambi. Hata hivyo, kanuni hizi zinaweza kutumika kwa urahisi kwa kufeli kwingine ambako sio dhambi.

#### Aina tatu za kufeli

1. Kufeli ambako sio dhambi
2. Kufeli ambako ni dhambi
3. Kufeli kunakosababisha dhambi

**6. Tanguliza Hoja A. Kuyashinda matatizo (dakika 2-3). . . . . ukurasa wa 29, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Eleza kuwa sehemu ya kwanza ya ukuaji tutakayojadili inahusiana na tatizo lililosababisha kufeli. Unaweza kurejelea kwa haraka hatua za kwanza tunazopaswa kuchukua kukabiliana na kufeli tulizojadili katika Sura ya 2.

Unaweza kurejelea tena mfano wa mwamba wa barafu na chati inayoambatana nayo katika Sura ya kwanza ya kozi hii. Mtu anayekabiliana na tatizo la juu hataona maendeleo yoyote ya kudumu. Hii ndiyo sababu nyingine kwa mtazamo wetu tunasisitiza kwa watu wenye matatizo yanayodhibiti maisha ya kumtegemea Yesu Kristo kama suluhisho la kweli kwa matatizo yao. Uhusiano wa mtu na Yesu Kristo uko “chini ya mwamba wa barafu,” sababu kuu ya matatizo yake yote.

Ikiwa wataanzia chini ya barafu, na kuanza kufanya mambo kwa njia ya Mungu badala ya njia yao wenyewe, wataanza kuona shida zao za juu zikizidi kuwa ndogo na mwishowe hupotea.

**7. Jadili Hoja A-1. Je, Mtazamo wangu juu ya kufeli ni upi? (Dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 29-30, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Waambie baadhi ya wanafunzi kuzungumzia baadhi ya mitazamo yao juu ya kufeli katika maisha yao.

Unaweza kuwakumbusha kwamba Kozi ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*, **Mitazamo**, inashughulikia mada hii kwa undani zaidi.

Andika orodha ya mitazamo ya kawaida ambayo wanafunzi wako wamekuwa nayo kuhusu kufeli.

Kisha jadili maana ya kuwa na mtazamo chanya kwa kufeli.


**8. Jadili Hoja A-2. Imani za uwongo na za ukweli (dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 31, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Eleza kwamba imani za uwongo zinaambatana na kufeli ambako kunahusiana na dhambi. Inaweza kuwa vigumu kwa baadhi ya wanafunzi wako kuelewa.

Waambie wanafunzi wako wataje baadhi ya imani za uwongo zinazoambatana na kufeli maishani mwao. Kuwa tayari kutoa mifano zaidi kutoka kwa maisha yako mwenyewe, au maisha ya watu wengine.

**9. Tanguliza Hoja A-3. Fahamu sababu, matokeo, na suluhisho la kila kufeli (dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 31-35, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Tumia chati ya “Kuelewa Kufeli Kwangu,” kwenye ukurasa wa 31 wa Mwongozo wa Mwanafunzi kuanzisha sehemu hii ya somo.



3

Eleza kwamba tunapoangalia yale yanayohusika katika kushinda matatizo, tunapaswa kuona kuwa kuna sehemu tatu kuu ambazo tunapaswa kuchunguza-sababu, matokeo, na suluhisho.

Ikiwa watazingatia mojawapo ya maswala haya matatu, watakosa sehemu kuu ya mchakato huu wa ukuaji. Mwanafunzi anaweza kusema, “Sijali ni nini kilichosababisha, ninataka suluhisho tu!”

Katika kuangalia sababu za matatizo yao, ni muhimu sana kuwajibikia matatizo yao. Huu sio wakati wa kuwalaumu wengine kwa matatizo yao.

**10. Jadili Hoja Ndogo A-3-a. Je, Mungu anataka nikabiliane aje na kufeli huku? (Dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 32, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Ni muhimu sana tusingitize kuwa mchakato wa kutatua shida zetu unahitaji Yesu. Huu ndio msingi wa njia mpya na yenye mafanikio ya kutatua shida zetu. Hatutoi mkakati wa kibinafsi wa kutatua shida zetu.

Unaweza kutumia mfano mmoja au miwili ya Kibiblia ya watu ambao walikabiliana na matatizo yao kwa kuomba msaada kutoka kwa Mungu.

**11. Jadili Hoja Ndogo A-3-b. Kukabiliana na matokeo ya kufeli kwangu (dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 32, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Taja kuwa matokeo ya kufeli kwetu ni tofauti na sababu za kufeli kwetu. Tunaweza kuchukua hatua mahususi kukabiliana na matokeo haya ya kufeli kwetu tunapotafuta ukuaji ambao Mungu ametupatia.

**12. Jadili Hoja Ndogo A-3-c. Je, ni hatua gani za kutekeleza suluhisho la Mungu kwa shida hii? (Dakika 7-10). . . . . ukurasa wa 33-35, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Katika kujadili suala hili ni vyema kuwasaida kuona kwamba ni lazima wachukue hatua maalum za ukuaji. Mara nyingi Wakristo wanya wanataka kupata suluhisho la haraka kwa matatizo yao.

Wahimiza kuona kwamba ukuaji halisi unaweza kuchukua muda na kazi ngumu sana. Tazama Mwongozo wa Mwanafunzi kwa maelezo zaidi juu ya maswala yanayojadiliwa hapa.

Tumia chati “Kukua Kupitia Kufeli Kwangu” (ukurasa 34, Mwongozo wa Mwanafunzi) kuonyesha kwamba hatua ndogo za maendeleo zinaweza kuhitajika wakati wanataka kushinda matatizo.



Baadhi ya wanafunzi wako wanaweza kuuliza wafanye nini wanapozidi kufeli katika sehemu ileile. Chati hii inaonyesha jinsi mtu anaweza kuendelea mbele huku akifeli. Wengine wanaweza kufeli kwa sababu mikakati yao ya kupona haifanyi kazi kwao. Watahitaji kurekebisha mikakati yao ya kupona.


Jambo la mwisho katika sehemu hii ya kufuata suluhisho la Mungu kwa matatizo ni Hoja ndogo 3. “Kuandaa mpango wa kupona” (Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 34). Inazungumzia kutenda mengi zaidi ya kuzungumzia jinsi ya kukabiliana na matatizo yao. Wanapaswa kuandika hatua watakazochukua kushughulikia tatizo fulani.

Waeleze wanafunzi wako kwamba “Mpango huu wa Urejesho” ni zaidi ya orodha ya hatua za kujisaidia kushinda kufeli kwao. Wanahitaji kumweka Mungu katika mpango huu. Je! Mungu anataka watumie nini kama hatua zao za kupona? Mungu anavutiwa na suluhisho halisi — mabadiliko ya kweli.

Itakuwa vyema kwao kujumuisha ahadi maalum kutoka kwa Mungu ambazo zinaendana na mpango wao wa kupona. Hakikisha kuwa kuna usawa hapa. Sitaki kufanya kile ambacho Mungu atafanya katika mchakato huu wa kupona. Lakini pia ni makosa kutarajia Mungu afanye ninachotakiwa kufanya.

**13. Jadili Hoja A-4. Kufeli kunanigusa**  
(dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 34-35, Mwongozo wa Mwanafunzi

Tumia chati ya “Kufeli Hunigusa,” katika ukurasa wa 35 katika Mwongozo Mwanafunzi ili kuwasaidia wanafunzi kuona kwamba kushindwa hutuweka katika nafasi mbalimbali.



Mfano huu unaweza kutumika katika sehemu mbalimbali katika kozi hii kwenye somo hili na katika masomo yote yaliyosalia katika kozi hii, haswa wakati tunashughulika na kurudia.

Kuna masuala kadhaa muhimu unayopaswa kuwaonyesha wanafunzi.

1. Jaribu au kichocheo hutufanya kuchagua. Tunaweza kuchagua njia ambayo ni bora kwa Mungu au tunaweza kuchagua kuanguka kwenye majaribu na kuyaruhusu kutuelekeza mbali na njia ya Mungu.
2. Wasaidie wanafunzi kuona kwamba kusikiliza jaribu hakusababishi kufeli mara moja, ila ni tunapochagua kufuata “njia zetu za zamani” tunaelekea kwa kufeli.
3. Hata wakati tunaposhindwa tunaweza kufanya uamuzi. Kadiri tunavyochukua muda mrefu kumgeukia Mungu ili kupata msaada, ndivyo tunavyozidi kwenda mbali na pale ambapo Mungu anataka tuwe. Taja kwenye kielelezo kwamba, mfano huu unaonyesha mtu huyo anavyozidi kuingia ndani ya matatizo yake kabla ya kumrudia Mungu ili amsaidie. Hili halipaswii kutokea. Mara tu tunapofeli, tunaweza kumwendea Mungu mara moja ili atusaidie.
4. Wakati tunapomwomba na kumwuliza Mungu atusaidie, yuko tayari kutusaidia. Lakini toba haiturudishi mara moja pale tunapohitaji kuwa.
5. Lazima tufanye juhudi za kurejea mahali ambapo Mungu anataka tuwe kila siku. Hatufanyii kazi msamaha wa Mungu — hilo hutendeka tunapokiri dhambi zetu. Lakini kuacha njia za zamani za dhambi na kuenenda kwa njia mpya za Kimungu ni mchakato — pia ni mchakato ulioinuka kama kielelezo kinavyoonyesha. Tutahitaji msaada wa Mungu katika mchakato huu wa kupona.

Tumia hadithi ya (1) Daudi na Bathsheba na (2) Adamu na Hawa kueleza kuwa kushindwa hutupeleka mahali pavya. Hatuzungumzii tu mabadiliko ya kijiografia. Tunazungumza pia juu ya mabadiliko ya maisha. Hatuwezi kurudi nyuma kwa wakati na kufuta kufeli na matokeo yake. Tunapaswa kuishi na matokeo hayo.

Jambo muhimu kwa wanafunzi wako kuona ni kuwa, lazima waweke macho yao kwa Yesu na wasogee karibu naye. Njia ya Mungu kujiondoa katika kufeli kwao sio kurudi nyuma kwa wakati-ni kusonga mbele pamoja Naye.

**14. Tanguliza Hoja B. Ishi maisha yenye afya  
(dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 35-38, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Ni vyema kutanguliza sehemu hii ifuatayo katika somo kwa kusema kwamba kukua kumfuta kufeli sio suluhisho la tatizo lililosababisha kufeli.

Kukua kwa kufeli kutakuwa sehemu ya maisha yao yote, ikiwa watakuwa watu ambao Mungu anataka wawe, basi — sio tu tatizo lililosababisha kufeli.

Hakikisha wanaelewa kuwa tunaposema, “Ishi maisha yenye afya,” tunazungumza zaidi ya afya kimwili.

Ikiwa somo hili linafundishwa katika kituo cha Changamoto kwa Vijana au programu sawiya ya kupona, utakuwa wakati mzuri wa kusema kwamba hatutafuti kutatua shida yao tu ya matumizi ya dawa—tuna lengo kubwa zaidi. Ufunguo halisi wa maisha ni kujifunza jinsi ya kumfuata Yesu katika kila sehemu ya maisha yako.

**15. Jadili Hoja B-1. Ninahitaji kufahamu mpango wa Mungu juu ya maisha yangu  
(dakika 2- 3). . . . . ukurasa wa 36, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Hii sio tu ya kufahamu mkondo wako wa kazi utakayofanya — tunapaswa kuwasaidia kuona kwamba Mungu anavutiwa na vitu vidogo vinavyoendelea katika maisha yao ya kila siku.

Cha mno hapa ni kwamba hatutoi mpango wa kujisaidia ili kuishi maisha bora. Tunatoa mpango wa Mungu kwa maisha bora. Hayo ndio maisha halisi!

**16. Jadili Hoja B-2. Endeleza nidhamu ya kumuishia Yesu  
(dakika 5- 10). . . . . ukurasa 36-37, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Sehemu hii ya somo inalenga kueleza maana ya kuwa mwanafunzi wa Yesu — kumfuata Yeye. Sehemu hii ya ukuaji ndio itazaa Mkristo aliyekomaa.

Onyesha kwamba Wakristo wengi wapya wametoka katika familia zilizo na matatizo. Mtazamo wao wa “maisha ya kawaida” unategemea maisha yao ya zamani ambayo hayakufaa. Mungu anawaita kuishi “maisha ya kawaida” kwa mujibu Wake. Jambo hili linaweza kuwa la kushangaza kwa wanafunzi kama vile lugha ya kigeni.

Kitabu bora ambacho kinaelezea hatua za kuishi maisha yenye afya kwa Mkristo ni *The Life Model: Living from the Heart Jesus Gave You: The Essentials of Christian living*, na James Friesen na waandishi wengine wanne. Kitabu kinapatikana mtandaoni.

Hakuna wakati katika kipindi hiki cha darasa, wa kupitia hatua zote za ukomavu zilizoko kwenye kitabu cha *The Life Model*, lakini itakuwa vyema kwa wanafunzi kufuatilia kibinafsi na kwa usomaji.

Katika kujadili sehemu hii ya somo, unaweza kutazama kwa kina Waefeso 4:1-3 na Waefeso 4:17-32. Mistari hii inazungumzia kile tunachopaswa kuweka mbali na kuacha katika maisha yetu mapya na Yesu.

**17. Jadili Hoja B-3. Kuweka mipaka ya kuishi maisha ya afya (dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 37-38, Mwongozo wa Mwanafunzi**

3

Suala hili la mipaka linaweza kuwa somo zima — au kozi nzima. Leo tunataka tu kutanguliza dhana hii na kuwasaidia kuona mipaka ni nini na jinsi inavyoweza kukabiliana na kufeli.

Dk Henry Cloud na Dk John Townsend wameandika msururu wa vitabu juu ya mipaka — ambavyo vinaweza kutumika kwenye mada hii.

Waulize wanafunzi wako aina ya mipaka wanayoweza kuweka katika maisha yao leo itakayowasaidia. Majibu yao yanaweza kukufahamisha kiasi cha uelewa wao juu ya suala hili na wanapohitaji kukua.

Eleza kwamba mipaka sio gereza la kukunyang'anya uhuru wako, lakini mipaka ni sehemu muhimu sana ya maisha ya kila Mkristo — sio kwa wale tu wanaokabiliana na kufeli.

**18. Tanguliza Hoja C. Chukua hatua za kuzuia kufeli tena (dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 38-40, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Rudia kwa haraka hatua 2 za kwanza za ukuaji ambazo tumezungumzia leo.

A. Kuyashinda matatizo

B. Ishi maisha yenye afya

Sehemu hii ya tatu na ya mwisho kujadiliwa leo inahusiana na kufeli walikofeli maishani mwao. Onyesha matatizo mawili hapa:

**Kwanza**, watu wengi hawataki kufikiria kuhusu matatizo yao yanapopita.

**Pili**, wanakosa kufahamu kwamba tuko kwenye vita vya kiroho, na Shetani yuko tayari kuwaangamiza kwa njia yoyote ile.

Sehemu hii inahusu ukweli — tunapaswa kujiandaa kwa vita ambavyo viko mbele yetu.



**19. Jadili Hoja C-1. Andaa mpango wa kuzuia kufeli tena (dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 39, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Wahimiza wanafunzi wako kuandika mikakati ya kuzuia kurudi nyuma. Wanapaswa kufahamu sehemu maalum zinazohitaji ukuaji ambazo watafanyia kazi, na pia kufahamu matatizo wanayoweza kukumbana nayo katika siku zijazo. Sasa, ni wakati wa kupanga mikakati hii, sio wakati wa kukabili jaribu.

Mkakati huu unajumuisha sehemu mbili:

1. La kufanya wakati unakabiliwa na jaribu au kichocheo.
2. Hatua za kuchukua kila siku kuzuia tatizo hili. Hizi ni hatua za kuishi maisha yenye afya, sio tu ujuzi wa kutatua matatizo.

Ni jambo moja kuandika mikakati, lakini ni kazi ngumu zaidi kuutekeleza mpango huo. Wahimiza wanafunzi kuishi maisha yao na Yesu.

Kwenye kurasa 54-66 katika kitabu, *Counseling for Relapse Prevention* na Terence T. Gorski & Merlene Miller (Herald House-Independence Press), kuna orodha ya hatua 37 za kurudia. Orodha hii ni muhimu kwa kuelewa njia hii ya kurudia. Pengine hautakuwa na wakati wa kujadili dalili hizo 37 za kurudia tena kwenye kipindi cha leo, hata hivyo, itakuwa vyema kuzungumzia haya kwa undani zaidi katika somo lingine ikiwa una wanafunzi ambao wamewahi kuwa na tatizo la ulevi maishani mwao.

Tafadhali kumbuka kuwa yaliyomo kwenye kitabu *Counseling for Relapse Prevention* hayajakubaliwa kabisa kutumika kwenye mpango wa Teen Challenge. Waandishi wa kitabu hicho wanazungumzia dhana ya ugonjwa wa uraibu kwa njia ambayo hailingani na kielelezo cha ufuasi wa Kikristo wa kushinda uraibu uliotumiwa katika Teen Challenge. Hata hivyo, mengi kuhusu kurudi nyuma na kuona katika kitabu hiki hayapingani na kile kinachoaminiwa kwenye Teen Challenge, na maswala mengi yaliyomo kwenye kitabu hiki ni ya kibiblia ingawa waandishi hawalinganishi.

Kila moja ya dalili 37 za kurudia zilizotajwa na Gorski na Miller pia, zinaweza kutumika kama malengo maalum ya kuona. Kwa mfano, kuchukua kila dalili na kuweka mikakati maalum ya kuona ili kukabiliana na dalili hiyo.

Ikiwa unachagua kutumia kipindi kingine cha darasa kushughulikia suala hili kwa undani zaidi, unaweza kuwaambia wanafunzi wako waorodheshe dalili zozote kati ya dalili 37 ambazo zimekuwa tatizo (au udhaifu) katika maisha yao. Kisha, unaweza kujadili ni hatua gani wanazoweza kuchukua ili kukua katika sehemu hizo ambazo zinawasaidia kukabiliana na dalili hiyo ya kurudia.

**20. Jadili Hoja C-2. Tambua vichocheo vinavyoweza kutokea (dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 40, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Suala hili la vichocheo linaweza kuwa somo zima. Tunachotaka kufanya hapa ni kutanguliza dhana ya kwasaidia kuona jinsi vichocheo vinaweza kuwasababishia kufeli.

Tumia sehemu hii ya somo kuwaeleza wanafunzi wako kuwa Mwongozo wa Somo Zoezi la 4, *Vichocheo vyako ni gani?* Hakikisha wanaelewa vichocheo nini na ni jinsi gani vinahusiana na matatizo yao. Zoezi hili linapaswa kukamilika kabla ya kipindi kijacho cha darasa.

Kwa habari ya ziada juu ya suala la vichochezi, soma nakala ya *Vichocheo vyako ni gani?* (*What are your triggers?*) na David Batty. Nakala hiyo iko katika sehemu ya Vifaa vya Huduma kwenye wavuti [www.iTeenChallenge.org](http://www.iTeenChallenge.org)

**3**

**21. Jadili Hoja C-3. Kuza mahusiano ya uwajibikaji (dakika 2-5). . . . . ukurasa wa 40, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Suala hili linaweza pia kuwa kipindi kizima cha darasa. Sisitiza hitaji la kuwa na angalau mtu mmoja wa kuwajibikia katika maisha yao. Mtu huyu anapaswa kuwa karibu ili waweze kukutana angalau mara moja kwa wiki.

Bainisha kuwa, uhusiano wa aina hii unaweza kuwa na athari kubwa katika kuwasaidia kushinda kufeli na kuishi kwa ushindi. Hata hivyo, itafanya kazi tu ikiwa ni waaminifu kabisa. Ikiwa watamficha mtu huyu siri, watakuwa wanajiandaa kufeli zaidi.

Kuwa na uhusiano wenye uwajibikaji sio kuwa na polisi maishani mwako. Tunapaswa kuona uhusiano wa aina hii kama urafiki na mtu anayekujali sana. Ni ishara ya upendo, sio kutoaminiana.

Ikiwa hupendi wazo la kuwajibika kwa mtu mwingine inaonyesha kutokomaa, sio nguvu yako.

**22. Matumizi binafsi (dakika 5-10)**

Kwa matumizi binafsi leo, wahimiza kuangalia kwa makini kufeli kwao. Waache wachague sehemu moja katika maisha yao na watathmini mahali walipo kwenye chati, "*Kukua Kupitia Kufeli Kwangu*". Tazama ukurasa 34 katika Mwongozo wa Mwanafunzi. Waambie waandike jambo moja au mawili wanayoweza kufanya kwa ufanisi ili kufuata njia ya Mungu ya kushinda kufeli huku. Unaweza kuwaambia watafute angalau andiko moja linalohusiana na suluhisho na waeleze jinsi mstari huu utawasaidia kukua.

**23. Kazi**

- A. Sahihisha Mwongozo wa Somo Zoezi la 3 *Kufeli Kwangu*.
- B. Wape kazi kutoka kwa Mathayo Zaburi 32:8-9 mwishoni mwa kipindi cha darasa.
- C. Waambie wanafunzi wako wasome Sura ya 4 katika Mwongozo wao wa Mwanafunzi ili kujandaa kuijadili katika kipindi kijacho cha darasa.

- D. Mwongozo wa Somo Zoezi 4, *Vichocheo vyako ni gani?* linapaswa kukamilika kabla ya kipindi kijacho cha darasa. Waeleze wanafunzi kuwa swali 1 lina nafasi ya majibu 7 na swali la 4 lina nafasi ya majibu 5. Haya yote ni majibu ya kibinafsi. Wanafunzi hawahitajiki kuwa na majibu 7 na 5 kwa maswali haya, hata hivyo mengi yanawahusu. Ikiwa hawana majibu, unaweza kujadiliana nao ili kuhakikisha wanaelewa maswala yanayoshughulikiwa katika zoezi hili.

#### 24. Tathmini ya somo

Hebu andika mawazo yako kuhusu jinsi ya kuboresha somo hili.

Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?

Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?

Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

## Somo la 4

### Kurudia uraibu

#### 1. Kweli Kuu ya Kibiblia

Mungu ana njia ya kuwaponya kwa kweli watu ambao wamerudia tena.

#### 2. Mstari Mkuu: 1 Wakorintho 10:13 Biblia Takatifu (SUV)

Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.

#### 3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili

Sura ya 4 katika Mwongozo wa Mwanafunzi inaendana na somo hili. Zoezi la 3 na 4 kwenye Mwongozo wa Somo linaweza kutumika katika somo hili.

#### 4. Maandalizi ya somo

Kipindi hiki cha darasa kimeundwa kushughulikia maswala kadhaa ya kimsingi yanayohusiana na kurudia. Somo hili la kurudia linaweza kuhitaji ufafanuzi mwanzoni, kulingana na historia ya wanafunzi wako. Ikiwa unafundisha kozi hii katika kituo cha Changamoto kwa Vijana au huduma sawia ambayo inafanya kazi na wale waliokuwa na matatizo kama uraibu, basi wanafunzi wako watafahamu neno kurudia ni nini.

Waeleze wanafunzi wako kwamba tunapotumia neno kurudia katika kipindi hiki cha darasa, tunazungumzia mchakato wa kurudi kwenye uraibu, kufeli, na tabia zingine ambazo zinatuweka mbali na wema wa Mungu kwa maisha yetu.

Ikiwa wanafunzi wako wamekuwa na historia ya uraibu, somo hili la kurudia litahitaji mafunzo ya kina ya zaidi ya kipindi hiki kimoja. Kozi moja ambayo inapatikana inaitwa *Kuelewa Hatua za Kurudia tena (Understanding the Steps to Relapse)*, na David Batty. Inapatikana katika wavuti ya [www.iTeenChallenge.org](http://www.iTeenChallenge.org).

#### 5. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5)

Anza kipindi cha darasa la leo kwa kutumia hadithi moja au zaidi ya mtu ambaye amerudia. Haya yanaweza kuwa mahojiano ya moja kwa moja. Yanaweza kuwa mahojiano ya video au hadithi ya mtu aliyerudia tena.

Mwambie mtu huyo azungumzie mambo ambayo yalisababisha kurudia na jinsi alivyohisi baada ya kurudia. Pia, mwambie mtu huyo aeleze jinsi alivyoona kutokana na kurudia.

**6. Jadili Hoja A. Sababu saba ni kwa nini uponaji wa haraka hugeuka kuwa kurudi tena (dakika 4-7). . . . . ukurasa wa 42-45, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Sababu hizi saba zinapaswa kujadiliwa kwa kina wakati huu. Tunataka tu wanafunzi wafahamu kuwa kuna sababu tofauti ambazo zinawafanya watu kurudia haraka baada ya kumaliza programu ya kupona.

Jambo lingine ambalo tunataka kuzungumzia mapema katika somo hili, ni kwamba kurudia ni kawaida, lakini kuna njia za kuizuia. Baadhi ya wanafunzi wako wanaweza kuogopa kurudia, na hofu yao inaweza kuwa na msingi-kulingana na maisha yao ya zamani.

Wengine wanajiamini kupita kiasi na hawaoni hii kama shida inayoweza kutokea katika maisha yao.

Kusudi letu hapa sio kuingiza hofu ndani yao, ila ni kufanya somo hili kuwa la ukweli. Kurudia kunaweza kuwa tatizo halisi katika maisha ya mtu yeyote ambaye amekuwa na uraibu au tatizo lililodhibiti maisha.

Ikiwa wanafunzi wako ni pamoja na wale ambao wamewahi kuwa waraibu, unaweza kuwauliza wajitolee kutoa majibu ili kuona ikiwa kuna yeyote kati yao ambaye amerudia baada ya kupitia programu ya kupona. Je! Kurudia kwao kunaambatana na sababu hizi 7, au kulikuwa na sababu tofauti ya kurudia kwao?

**7. Jadili Hoja B. Ni nini husababisha kurudia tena uraibu? (Dakika 7-10). . . . . ukurasa wa 45-46, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Unapojadili mambo matatu makuu yaliyoorodheshwa katika Mwongozo wa Mwanafunzi, chukua muda kutoa mfano kwa kila sababu.

Wakati unajadili Hoja B-2, **“Kushindwa kushughulikia shida za kale”** — hakikisha wanaelewa umuhimu wa kuwa na njia za kimungu za kutatua tatizo. Mawazo ya kichawi yanaweza kumfanya mtu kuamini kwamba wanachohitaji kufanya ni kumwamini Yesu na kuomba, na kila kitu kitakuwa sawa. Lakini hilo si kweli. Kuishi maisha ya Kikristo ni maisha ya kila siku — ambayo yanahitaji nidhamu na uvumilivu. Tazama Yakobo 1:2-5.

Ikiwa haya yanafundishwa kwenye programu ya Changamoto kwa Vijana au programu sawia ya urejesho, basi wasilisha Hoja B-3 kwa njia iliyo wazi — kurudia kunaweza kusababishwa na kushindwa kushughulikia uraibu na matatizo yanayodhibiti maisha. Sisitiza umuhimu wa kufungua maisha yao yote kwa Kristo, sio shida zao za dawa za kulevya tu.

**8. Jadili Hoja C. Kuelewa kurudia uraibu tena (dakika 7-10). . . . . ukurasa wa 46-48, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Unapojitayarisha kujadili jambo hili, waeleze wanafunzi wako kuwa maswala mengi katika sehemu hii ni sawa na maswala ambayo tuliangalia hapo awali katika kozi hii. Kurudia ni aina moja ya kufeli — ambapo, mtu ambaye amewahi kufeli hapo awali, alisaidiwa na akapiga hatua za kupona, halafu akarudia tabia ile ile au nyingine ya uharibifu tena.

Kwa kujadili sehemu hii ya somo, unapaswa kutathmini maisha na kiwango cha ufahamu juu ya kurudia. Masuala haya matatu yaliyoshughulikiwa hapa yanahusiana.

1. Njia ya uraibu ni ipi?
2. Kupona ni nini?
3. Kurudia uraibu ni nini?

Katika kujadili maswala haya matatu, ni muhimu kuona jinsi kufeli na matatizo yanaambatana na mwaswala haya matatu. Wengi walianza na uraibu kama njia ya kutibu maumivu waliyokuwa wakipata kwa sababu ya matatizo maishani mwao.

Ikiwa hawatajifunza njia mpya za kimungu za kutatua shida zao, wanaweza kurudia baadaye maishani.

Unapozungumza juu ya kurudia, ni muhimu kuona dalili zinazoendelea. Terence Gorski na Merlene Miller wameandika vitabu kadhaa juu ya kurudia ikiwa ni pamoja na *Counseling for Relapse Prevention*. Unapaswa kufahamu kuwa wanawasilisha maandishi yao yote kutoka kwa kielelezo cha matibabu ya ugonjwa wa uraibu, hata hivyo, mengi wanayosema juu ya kurudia tena ni sawa sio kwa walevi tu, bali kwa uraibu wowote ule.

Kwenye kurasa za 54-66 kitabu, *Counseling for Relapse Prevention* na Terence T. Gorski & Merlene Miller (Herald House-Independence Press), kuna orodha ya hatua 37 za kawaida za kurudia. Orodha hii ni rasimali bora ya kuelewa njia hii ya kurudia. Pengine, hautakuwa na wakati wa kutosha katika somo lako leo kujadili dalili hizo 37 za kurudia, lakini itakuwa vizuri kujadili kwa undani zaidi katika somo lingine ikiwa una wanafunzi ambao wamewahi kuwa waraibu maishani mwao.

Tafadhali kumbuka kuwa yaliyomo kwenye kitabu *Counseling for Relapse Prevention* hayajakubaliwa kabisa kutumika kwenye Changamoto kwa Vijana. Waandishi wa kitabu hicho wanazungumzia dhana ya ugonjwa wa ulevi kwa njia ambayo hailingani na kielelezo cha ufuasi wa Kikristo wa kushinda uraibu uliotumiwa katika Changamoto kwa Vijana. Hata hivyo, mengi kuhusu kurudi nyuma na kupona katika kitabu hiki hayapingani na kile kinachoaminiwa kwenye Changamoto kwa Vijana, na maswala mengi yaliyomo kwenye kitabu hiki ni ya kibiblia ingawa waandishi hawalinganishi.

**9. Tanguliza Hoja D. Ni nini cha kufanya ikiwa kurudia tena uraibu kunatokea (dakika 3-5). . . . . ukurasa wa 49-51, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Katika kutanguliza sehemu hii ya kurudia tena, ni muhimu uweke msingi sahihi wa sehemu hii ya somo.

**Kwanza**, mtu yeyote aliye na historia ya uraibu ana uwezo wa kurudia-hata ikiwa amekuwa safi kwa miaka mingi.

**Pili**, hatutaki kutoa maoni kwamba kila mtu hurudia, kwa hivyo sio jambo kubwa. Kurudia ni uharibifu-kamwe sio chaguo nzuri.

**Tatu**, Mungu bado anawapenda hata wakirudia. Naye anasimama tayari kuwasaidia kurudi kwenye njia ya kupona.

**Nne**, baadhi ya wale ambao wamewahi kuwa waraibu wanaweza kuwa wamepata muujiza wa ukombozi-ambapo Mungu aliwaponya mara moja na hawakupitia tatizo lolote la kuacha uraibu. Ikiwa watarejea, haitakuwa dhahiri kwamba Mungu atafanya muujiza mwingine kama huo. Kwa kweli, kuna wengi ambao wametarajia hilo, na kugundua kuwa mara ya pili Mungu hakufanya muujiza kama huo. Mungu bado yuko tayari kukusaidia, lakini unaweza kuwa mchakato tofauti wakati mwingine.

**10. Jadili Hoja D. Ni nini cha kufanya ikiwa kurudia tena uraibu kunatokea (dakika 10-15). . . . . ukurasa wa 49-51, Mwongozo wa Mwanafunzi**

Unapowasilisha hoja sita katika sehemu hii, utaona kuwa zingine ni sawa na yale tuliyoyazungumzia hapo awali katika kozi hii wakati walikabiliana na kufeli. Jinsi wanapaswa kukabiliana na kurudia ni sawa na jinsi ya kukabiliana na kufeli kwingine. Wanapaswa kuwa makini sana wanapounda tena mikakati yao ya kupona.

Unaweza kutumia Mwongozo wa Somo Zoezi 4, *Vichocheo vyako ni gani?* katika sehemu hii ya somo. Kukabiliana na kurudia kunamaanisha kuelewa vizuri jinsi vichocheo vinawavuta tena kwenye uraibu wao.

Hakikisha kurudia tena kunakabiliwa kwa usawa. Hatutaki kupunguza uzito wa kurudia. Kwa upande mwingine, hatutaki kutoa maoni kwamba ikiwa watarudia, basi mafunzo haya yote ya Mungu kuwasaidia ni ya uwongo.

Kinyume kabisa. Msaada wa Mungu ni wa kweli, na njia zake hufanya kazi. Kile lazima mtu huyu afanye ni kuwajibikia kikamilifu kurudia kwake na kisha afanye bidii ya kupona. Yesu yuko tayari kumsaidia —Hatachukuwa jukumu lako, mbali atafanya jukumu lake.

Yesu alisema ikiwa unataka kuwa mwanafunzi Wake lazima uje, uchukue msalaba wako na umfuata. Kuchukua msalaba wako sio fimbo ya kufanya miujiza— inazungumzia changamoto ngumu ya kumfuata Yesu.

Hakikisha unafunga somo hili kwa ujumbe mzito wa matumaini. Haijalishi wamerudia mara ngapi, Mungu yuko tayari kuwasaidia kukua. Vita vinafaa kupiganwa. Lazima wantazame Yesu.

Hakikisha kwamba wanafunzi wako wanaelewa kuwa hata kama wamefeli hawajapoteza wokovu wao. Ibilisi anaweza kuwalundikia kila aina ya lawama wanapofeli, na anaweza kuwaambia wamepoteza yote. Lakini unapaswa kusaidia wanafunzi wako kuona kwamba Mungu bado anawapenda bila kujali ni mara ngapi wamefeli. Cha mno ni kuamka na kumwomba Mungu akusamehe, na kisha uanze kuzingatia jinsi ya kumkaribia Mungu na kukua katika sehemu ambazo zinahitaji kuimarika.

### 11. Matumizi Binafsi (dakika 5-7)

Waambie wanafunzi waandike mambo 5 watakayofanya ili kuzuia kurudia katika maisha yao. Unaweza kuwaweka wawili wawili na watoe majibu yao, na kisha waombeane.

### 12. Kazi

Sahihisha Zoezi 4 Mwongozo wa Somo, *Vichocheo vyako ni gani?* Swali 1 lina nafasi ya majibu 7 na swali la 4 lina nafasi ya majibu 5. Haya yote ni majibu ya kibinafsi. Wanafunzi hawahitajiki kuwa na majibu 7 na 5 kwa maswali haya, hata hivyo, mengi yanawahusu. Ikiwa hawana majibu, unaweza kujadiliana nao ili kuhakikisha wanaelewa maswala yanayoshughulikiwa katika zoezi hili.

### 13. Tathmini ya somo

Hebu andika mawazo yako kuhusu jinsi ya kuboresha somo hili.  
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?  
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?  
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?



## Somo la 5

### Mtihani

#### 1. Utangulizi

Fanya utangulizi wa somo litakalofuata.

- A. Wape Mwongozo wa Somo au Mazoezi yoyote ambayo yanapaswa kukamilishwa kabla ya kipindi cha kwanza cha kozi ifuatayo utakayofundisha.
- B. Waelekeze wanafunzi kufungua ukurasa wa mwisho katika Mwongozo wa Somo Lipya. Wanapaswa kupata nakala safi ya *Orodha ya Kazi za Darasani*. Wape tarehe za majaribio ya chemsha bongo, Zoezi, na mtihani.
- C. Wape Mwongozo wa Mwanafunzi mpya na uwaambie kurasa watakazosoma kabla ya kipindi kifuatacho darasani.

#### 2. Wape mtihani wa Somo hili.

#### 3. Ikiwa hujafanya hivyo bado, rudisha chemsha bongo zote na mazoezi ambayo umesahihisha.



## Mwongozo wa Mwanafunzi

Mwongozo wa Mwanafunzi Haujajumuishwa kwenye hati hii,  
lakini unapatikana katika hati tofauti.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari  
kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Mwanafunzi.

## Mwongozo wa Somo

Haukujumuishwa kwenye hati hii, lakini unapatikana katika hati tofauti.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Somo.

**Mtihani**  
**Majibu ya mtihani**  
**Cheti cha Somo**

Tazama ukurasa wa 5 wa mwongozo huu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mtihani na cheti.



Jina \_\_\_\_\_

Kukua Kupitia Kufeli

Tarehe \_\_\_\_\_

Mtihani Toleo la 5

Darasa \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_ Alama

**Maswali Ya Kweli au Si Kweli** (Alama 1 unusu kwa kila moja)

**Maelekezo:** Weka alama ya  X  ikiwa jibu ni kweli.

Weka alama ya  O  ikiwa jibu si kweli.

1. \_\_\_\_\_ Kila mara mtu anatenda dhambi anapofeli.
2. \_\_\_\_\_ Mungu anakukasirikia kila unapotenda dhambi.
3. \_\_\_\_\_ Mungu ameahidi kukusamehe iwapo unapomwomba msamaha kwa dhati.
4. \_\_\_\_\_ Iwapo nitafeli, kamwe sipaswi kukubali kuwa nimekosa.
5. \_\_\_\_\_ Wakristo waliofaulu kamwe hawafeli katika lolote.
6. \_\_\_\_\_ Ninapomwomba Mungu anisamehe kwa kutenda dhambi, ninapaswa kufanya uamuzi wa kuacha kutenda hiyo dhambi.
7. \_\_\_\_\_ Kila mara napaswa kujaribu kutafuta kilichosababisha kufeli kwangu.
8. \_\_\_\_\_ Kuvuta sigara ni tatizo la shina.
9. \_\_\_\_\_ Shina linalosababisha matatizo yangu ni kufanya mambo kwa njia yangu badala ya kufuata njia ya Mungu.
10. \_\_\_\_\_ Kutokuwa na usalama ni matokeo ya kawaida ya kuweka thamani yetu katika vitu vya kimwili.
11. \_\_\_\_\_ Mtu anayekosoa sana kwa kawaida ana shina katika tatizo la uchungu.
12. \_\_\_\_\_ Ninapoomba mtu msamaha, kila mara ninapaswa kutangulia kusema, "Iwapo nimekosa, tafadhali nisamehe."
13. \_\_\_\_\_ Sipaswi kusamehe mtu isipokuwa amelipa alichoniibia.
14. \_\_\_\_\_ Njia bora zaidi ya kuomba msamaha ni kuandika barua na kumwomba mtu akusamehe.
15. \_\_\_\_\_ Iwapo unaendelea kuanguka, hili linaonyesha kuwa haukui kamwe katika eneo hilo la maisha yako.
16. \_\_\_\_\_ Wakristo kamwe hawahisi kuchoshwa na mtu au kitu.
17. \_\_\_\_\_ Daima ni mapenzi ya Mungu nimsamehe mtu aliyenikosea mimi, hata yeye asipokubali makosa yake.
18. \_\_\_\_\_ Hatua ya kwanza ya kurudi nyuma ni wakati mtu anarejea kama kawaida kutumia mihadarati, pombe au chochote kile alichokuwa ametawaliwa nacho.
19. \_\_\_\_\_ Mtu hawezi kurudi katika kutawaliwa na tabia fulani wasipokuwa kwanza wamepata nafuu.
20. \_\_\_\_\_ Iwapo nina ubishi na mtu, ninapaswa kumwomba anisamehe hata kama ninajua kuwa sikuwa na makosa.





---

2. Ni matatizo yapi matatu ya shina ambayo ndiyo shina la matatizo yetu yote?  
(alama 6, kila sehemu alama 2)

1. \_\_\_\_\_

2. \_\_\_\_\_

3. \_\_\_\_\_

3. Ni shina lipi moja ambalo ndilo sababu ya matatizo yangu? (alama 4)

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

4. Toa mfano wa kile kilichotendeka ulipomwendea mtu mmoja wiki hii na ukamwomba akusamehe.

A. Ulisema nini ulipomwomba mtu huyu akusamehe? (alama 5)

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

B. Je, mtu huyo aliitikia vipi? (alama 5)

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

C. Ulihisi vipi baada ya kusamehewa? (alama 5)

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

D. Ulijifunza nini kutokana na uzoefu huo? (alama 3)

1. \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

2. \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

3. \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

5. Ni yapi maeneo matatu ya kukua katika hali ya kukua kupitia kwa kufeli?  
(Alama 6, kila sehemu alama 2)

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_

**6. Mfano wa Kujifunzia**

Debora alibadilika kuwa Mkristo miezi minne iliyopita. Anahisi kuwa na hatia kwa sababu aliiba dola 100 kutoka kwa rafiki yake kabla hajawa Mkristo.

- A. Debora anapaswa kufanya nini? (alama 5) \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_

- B. Debora anapaswa kumwambia rafiki yake nini?  
Andika maneno halisi anayoweza kumwambia rafiki yake. (5 alama)

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

7. A. Toa mfano mmoja kuhusu kufeli katika maisha yako. (alama 4)

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

- B. Ni hatua zipi unazochukua ili ukue na hata usifeli tena katika eneo hili?  
(alama 8, kila sehemu alama 2)

1. \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_

**Kukua Kupitia Kufeli**  
**Mtihani Wa 5**  
**Karatasi ya Majibu**

**Ukurasa 1**

**Maswali ya Kweli-Sio Kweli**  
(Alama 1 kwa kila moja)

1.  Si Kweli
2.  Si Kweli
3.  Kweli
4.  Si Kweli
5.  Si Kweli
6.  Kweli
  
7.  Kweli
8.  Si Kweli
9.  Kweli
  
10.  Kweli
  
11.  Kweli
12.  Si Kweli
  
13.  Si Kweli
14.  Si Kweli
15.  Si Kweli
  
16.  Si Kweli
17.  Kweli
  
18.  Si Kweli
  
19.  Kweli
  
20.  Kweli

**Ukurasa wa 2**

**Maswali ya Kuchagua Kati ya Majibu Mengi** (Alama 2 kwa kila moja)

1.  B
  
2.  C
  
3.  A
  
4.  A
  
5.  B

**Maswali ya Simulizi Fupi**

1. Alama 14  
Mathayo 6:14-15    Zaburi 32:8-9

**Ukurasa wa 3**

2. Alama 6 (Alama 2 kwa kila sehemu)

1. Uchungu
2. Maadili ya kuthamini mali
3. Uasherati

3. Alama 4 Jibu lililopendekezwa

Kufanya mambo kwa njia yangu badala ya kufanya mambo kwa njia ya Mungu.

(Jibu mbadala)

Kupinga au kukataa mapenzi na nguvu ambazo Mungu anakupatia kukabili maisha jinsi anavyotaka nifanye.

**Kukua Kupitia Kufeli**  
**Mtihani Wa 5**  
**Karatasi ya Majibu**

**Ukurasa wa 3** (unaendelea)

4. A. Jibu la Binafsi (Alama 5)
- B. Jibu la Binafsi (Alama 5)
- C. Jibu la Binafsi (Alama 5)
- D. Alama 3 (Kila moja 1)
  1. Jibu la Binafsi
  2. Jibu la Binafsi
  3. Jibu la Binafsi

**Ukurasa wa 4**

5. Alama 6 (Alama 2 kila sehemu)  
Majibu yaliyopendekezwa
  1. Shinda tatizo.
  2. Ishi maisha yenye afya.
  3. Chukua hatua kuzuia kufeli tena.
6. A. Jibu la Binafsi (Alama 5)
- B. Jibu la Binafsi (Alama 5)
7. A. Jibu la Binafsi (Alama 4)
- B. Alama 8 (Alama 2 kwa kila sehemu)
  1. Jibu la Binafsi
  2. Jibu la Binafsi
  3. Jibu la Binafsi
  4. Jibu la Binafsi

# Hongera

Amemaliza

## Kukua Kupitia Kufeli

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya  
na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio  
utaendelea na masomo yako yajayo.

Wakufunzi \_\_\_\_\_

Tarehe \_\_\_\_\_

# Hongera

Amemaliza

## Kukua Kupitia Kufeli

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya  
na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio  
utaendelea na masomo yako yajayo.

Wakufunzi \_\_\_\_\_

Tarehe \_\_\_\_\_

